# Nipashe

Jumamosi Februari 19, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580861
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

SportPesa
TZS. 940,850,660
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Ziara** ya Rais Samia Ufaransa yaleta tija nchini

UKURASA 8



RAIS LALIGA AMWITA MBAPPE

UKURASA 22



Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, akiwaaga wanachama na wapenzi wa chama hicho wakati akitoka katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, Dar es Salaam jana.

# Mashahidi 28 kujenga utetezi kesi ya Mbowe

• **Ni** pamoja na vielelezo 35, wakutwa na kesi ya kujibu Mahakama Kuu... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### BABU MIAKA 89 MBARONI TUHUMA KUNAJISI MJUKUU

JESHI la Polisi Mkoa wa Geita linamshikilia Gervas Katemi (89), mkazi wa Kijiji cha Nyamisebeyi wilayani Biharamuro...

UKURASA WA 3

### MISHAHARA HEWA BADO TATIZO NCHINI

BUNGE limesema limebaini ujanja kwa fedha nyingi kutoka Hazina kwenda halmashauri kuliko kiasi...

UKURASA WA 4

### SPIKA TULIA AWAONYA MAWAZIRI

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amewataka mawaziri na manaibu wao kuhudhuria ipasavyo vikao vya Bunge...

## Mawakili waitetea hukumu ya Sabaya

UKURASA 5





Wanachama na wapenzi wa Chadema wakimpungia mikono Mwenyekiti wao, Freeman Mbowe, wakati anatoka katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, Dar es Salaam jana. **PICHA ZOTE: MIRAJI MSALA**

## Bunge laingilia kati deni kubwa ATCL

UKURASA 2





MICHEZO SIMBA YAZIPIGIA HESABU POINTI 6 UK.24 MAONI, KATUNI UK.6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza katika Kikao na Wakuu wa Mikoa kwa njia ya mtandao kuhusu Sensa ya Watu na Makazi akiwa Ofisini kwake Mlimwa jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Mashahidi 28 kujenga utetezi kesi ya Mbowe

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi imewaona Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, na wenzake watatu wana kesi ya kujibu katika mashtaka matano ya ugaidi yanayowakabili.

Mahakama imemwachia huru mshtakiwa wa kwanza Halfani Bwire kwa shtaka la sita baada ya kuona hana kesi ya kujibu. Shtaka hilo linahusu kukutwa na vifaa vya jeshi zikiwamo sare za Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

Uamuzi wa mahakama ulitolewa jana mbele ya Jaji Joachim Tiganga baada ya kupitia ushahidi uliotolewa na mashahidi 13 wa upande wa mashtaka na vielelezo 39.

Akisoma uamuzi huo, Jaji Tiganga alisema Mahakama ilipitia ushahidi ulioletwa na upande wa mashtaka kwa maneno na vielelezo ili kupima na kuona kama una chochote cha kuifanya iwatake washtakiwa kujitetea.

Jaji alisema katika shtaka la kwanza, washtakiwa wote wanadaiwa kati ya Mei Mosi na Agosti 5, 2020 maeneo ya Hoteli ya Aishi, mkoani Kilimanjaro, washtakiwa walikula njama ya kutenda vitendo vya ugaidi, kulipua vituo vya mafuta na mikusanyiko ya watu kwa lengo la kusababisha hofu kwa Watanzania.

Kosa la pili inadaiwa washtakiwa wote wanne walikula njama za kutenda kosa la kumjeruhi aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya na lengo ilikuwa kuleta hofu kwa Watanzania.

Kosa la tatu kwa mshtakiwa wa nne Mbowe, anadaiwa katika mikoa ya Morogoro na Dar es Salaam alitoa fedha Sh 6,999 kwa washtakiwa wengine akijua zitatumika kwa ajili ya kuwapata wahusika kwa ajili ya kulipua vituo vya mafuta Mwanza, Dar es Salaam, Arusha lengo ikiwa ni kuleta madhara kwa Watanzania.

Shtaka la nne kwa washtakiwa wote kwa pamoja wanadaiwa katika maeneo ya Aishi Hoteli mkoani Kilimanjaro, Dar es Salaam, Morogoro na Arusha, walishiriki kikao cha nia ya kupanga ugaidi na wanadaiwa walipanga kulipua vituo vya mafuta, mikusanyiko ya watu na vitendo hivyo vililenga kuleta hofu na madhara kwa raia.

Katika shitaka la tano, mshtakiwa wa pili, Adamu Kasekwa, anadaiwa Agosti 5, 2020 katika eneo la Rau Madukani, alikutwa na bastola aina ya Ruger A 5340 ikiwa na risasi tatu kwa lengo la kusaidia utendaji wa vitendo vya ugaidi kwa kulipua vituo vya mafuta na mikusanyiko katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Arusha.

Shitaka la sita, Halfani Bwire, ambaye ni mshtakiwa wa kwanza, anadaiwa Agosti 10, 2020 eneo la Kilakala wilayani Temeke, alikutwa akimiliki vifaa kadhaa vya jeshi zikiwemo sare za JWTZ na JKT.

"Kwa kipindi chote cha kesi mawakili wa serikali walikuwa 8 huku utetezi kwa ujumla wakiwa 19. Jukumu la mahakama ni kupitia ushahidi ili kujua kama kuna kesi au la. Mahakama imepitia ushahidi wote wa maneno na vilelezo ili kujibu swali moja kama washtakiwa wana kesi ya kujibu au la.

"Katika hatua hii ya kuangalia washtakiwa wana kesi au la, mahakama inatakiwa iangalie ushahidi kwa ujumla wake na haitakiwi iangalie kupima mashahidi kwa uzito wake.

"Katika shauri hili mahakama imetumia muda wa siku mbili kwa ajili ya kupitia ushahidi wote kuanzia shahidi wa kwanza hadi wa 13 na vielelezo vyote 39 na vile vitano vya utetezi," alisema Jaji Tiganga.

Alisema katika uamuzi kwa shtaka la sita, linalomkabili Bwire la kukutwa na vifaa vya jeshi, ushahidi ulioletwa ambao ulikuwa ni vielelezo hivyo, mahakama ilikataa kwa sababu upande wa mashtaka ulikiuka maelekezo ya sheria ya ukamataji na hakuna ushahidi ambao umeletwa mahakamani kwa ajili ya mshtakiwa kujitetea.

"Kwa shtaka la sita, mshtakiwa Bwire hana kesi ya kujibu, hivyo inamwachia huru. Kwa shtaka la kwanza, pili, tatu, nne na tano, mahakama imefanya uchambuzi na imepitia vielelezo. Katika hatua hii, mahakama imeona upo ushahidi umeleta tuhuma dhidi ya washtakiwa, hivyo wana kesi ya kujibu katika mashtaka matano.

"Wanatakiwa walete utetezi, wanaweza kujitetea wenyewe au kuleta mashahidi na wanaweza kukaa kimya au wanaweza kutoa ushahidi wao kwa kiapo au bila kiapo," alisema.

Baada ya kumaliza kusoma uamuzi, Jaji alitoa nafasi kwa upande wa utetezi kueleza utaratibu wa utetezi ndipo Wakili Jeremiah Mtobesya akadai kuwa wamepokea uamuzi na kwamba mshtakiwa wa kwanza ana kosa la kujibu katika shtaka la kwanza, pili na la nne, hivyo atajitetea mwenyewe chini ya kiapo na anatarajia kuita mashahidi wengine watano na yeye atakuwa wa sita na vielelezo vitano.

Wakili John Mallya kwa niaba ya mshtakiwa wa pili, Kasekwa ambaye amebaki na shtaka la kwanza, pili, nne na la tano ambalo anashtakiwa pekee yake, anatarajia kuleta mashahidi watatu na yeye atakuwa wa nne pamoja na vielelezo vinne.

Wakili wa mshtakiwa wa tatu, Ling'wenya, Fredrick Kihwelo, alidai mteja wake atajitetea kwa kiapo, atakuwa na mashahidi sita na vielelezo sita wakati Wakili Peter Kibatala akidai Mbowe atajitetea chini ya kiapo na atakuwa na mashahidi 10 na mwenyewe 11 pamoja na vielelezo 20.

Kutokana na uamuzi huo uliowakuta wana kesi ya kujibu, washtakiwa wataanza kujitetea Machi 4, mwaka huu.

# Bunge laingilia kati deni ATCL

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

BUNGE limeitaka serikali kukamilisha mchakato wa majadiliano baina ya Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) na Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA) ili kasoro zinazosababisha hasara ziondolewe.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Naghenjwa Kaboyoka, akiwasilisha juzi bungeni taarifa ya mwaka 2020/21, alisema Bunge linataka suala hilo kukamilika ndani ya mwaka huu kama serikali ilivyoiahidi kamati.

"Uchambuzi wa kamati ulibaini kuwa ATCL ilikuwa na mtaji hasi kiasi cha Sh. 246,665,705,000 (bilioni 246.666), huku ikiwa na changamoto za mtaji na deni linaongezeka kwa Sh. 152,165,868,000 zikiwamo Sh. 70,940,850,905 (asilimia 47 ya deni lote) inazodaiwa na TGFA.

Alisema walifanya uchambuzi na kubainia ATCL ilipata hasara ya zaidi Sh. bilioni 60.2 kwa mwaka 2019/20 na kufanya hasara jumuifu kuwa zaidi ya Sh. bilioni 152.1 tangu mwaka 2015/16.

"Uwapo wa madeni ya muda mrefu ni kihatarishi cha uendelevu wa kampuni kwa siku zijazo. Changamoto nyingine ni kutofikiwa malengo ya fedha kwa kiwango cha asilimia 76, kwa kuwa mwaka 2019/20 ulilenga kupata mapato ya zaidi ya Sh. bilioni 661.6 na kupata Sh. bilioni 157.6 kiasi cha kuathiri ufanisi wake," alisema.

Kaboyoka alisema walibaini uwapo wa vifungu vya kimkataba vinavyosababisha ATCL kuongeza deni hasa kwenye mkataba wake na TGFA kama kukodisha ndege ambazo hazikufanya kazi wakati wa janga la UVIKO-19 kwa zaidi ya Sh. bilioni 15.5, na wasingestahili kutozwa gharama hizo.

"Tulibaini ATCL iligharamia mara mbili matengenezo ya ndege zaidi ya Sh. bilioni 16.9 kutokana na dosari za kimkataba. Haya ndiyo yaliyochangia kutofikiwa malengo na ufanisi wa ATCL kwa mwaka wa fedha 2019/20," alisema.

# Mishahara hewa bado tatizo

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

BUNGE limesema limebaini ujanja kwa fedha nyingi kutoka Hazina kwenda halmashauri kuliko kiasi kilichopangwa, jambo linaloashiria uwapo wa mishahara hewa serikalini.

Vilevile, limesema lilibaini mishahara inayotolewa na Hazina ni mikubwa kuliko mahitaji ya halmashauri husika.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Grace Tendegu, akiwasilisha bungeni juzi taarifa ya mwaka 2021/22, alisema kuna 'madudu' mengi ya matumizi mabaya ya fedha za umma.

"Serikali ichunguze sababu za kutofautiana kwa mahitaji ya kiasi cha mishahara kati ya halmashauri za Mkoa wa Tabora na Wizara ya Fedha. Serikali ihuishe mfumo wa mishahara unaotumiwa na hazina uwe na mawasiliano na mfumo wa mishahara unaotumiwa na mamlaka za serikali za mitaa nchini, ili kupata kiasi sahihi cha mishahara inayopaswa kulipwa," alisema.

Tendegu alisema pendekezo hilo linakusudia kudhibiti kuibuka upya kwa hoja ya mishahara hewa na kuleta hasara bila sababu za msingi, kwa kuwa halmashauri ndiyo zenye kanzidata ya idadi halisi ya watumishi walioko maeneo yao.

"Kuna viashiria vya kuibuka tena kwa mishahara hewa serikalini. Kuna ushahidi kwamba kiasi cha mishahara kinachotolewa na Hazina huwa ni kikubwa kuliko kile kinachotakiwa katika halmashauri," alionya.

Mwenyekiti huyo alisema walibaini katika Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, mahitaji ya ni Sh. 13,162,727,251, lakini Hazina ilitoa Sh. 13,308,458,790, hivyo kusababisha ziada ya Sh. 145,731,539.

Alisema mahitaji ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua yalikuwa Sh. 17,679,189,899 lakini Hazina ilipeleka Sh. 17,889,094,180, hivyo kuwa na ziada ya Sh. 209,902,281.

Tendegu alisema kuwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Uyui, mahitaji yalikuwa Sh. 17,061,985,326 lakini Hazina ilipeleka Sh. 17,371,325,530, hivyo kuwa na ziada ya Sh. 309,340,200.

Alisema kamati ilijiridhisha kuwa serikalini kuna usimamizi hafifu wa mfumo wa mishahara na kwamba udhaifu huo usipodhibitiwa, utaibua upya mishahara hewa.




Mkazi wa Mtaa wa Kipunguni jijini Dar es Salaam, Said Juma, akichangia hoja katika mkutano wa kujadili mbinu za kukomesha vitendo vya ukeketaji ndani ya jamii uliofanyika eneo hilo juzi, kwa uratibu wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP). **PICHA: SABATO**

# Babu miaka 89 mbaroni tuhuma kunajisi mjukuu

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

JESHI la Polisi Mkoa wa Geita linamshikilia Gervas Katemi (89), mkazi wa Kijiji cha Nyamisebeyi wilayani Biharamuro kwa tuhuma za kumnajisi mjukuu wake, msichana mwenye umri wa miaka 17.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi mkoani Geita, Henry Mwaibambe, alidai tukio hilo lilitokea Febuari 5, mwaka huu pale Modesta Katemi (54), mkazi wa Magogo alipopigiwa simu na baba yake mzazi, Gervas Katemi (89), akimtaka amtumie wajukuu zake wakamsaidie kazi za mgahawani huko Biharamuro.

Mwaibambe alisema ndipo wajukuu wawili ambao ni Grace Tano (20), mkazi wa Magogo na mdogo wake (jina tunalo -17) waliruhusiwa kwenda huko na walifika siku hiyo hiyo nyumbani kwa babu yao huko Biharamuro.

Alisema ilipotimu majira ya saa mbili usiku, babu huyo anadaiwa alimfuata mjukuu mwenye umri wa miaka 17 alikokuwa amelala na kuanza kumbaka.

"Binti huyo alipiga kelele na 'wanazengo' (wakazi wa eneo hilo) walifika na kumkamata mzee huyo wa miaka 89 na kumpeleka Kituo cha Polisi Geita ili sheria ichukue mkondo wake," alisema.

Vilevile, Jeshi la polisi Mkoa wa Geita linamshikilia Bahati Marko (26), mkazi wa Kijiji cha Bugomba, Rulembela, Tarafa ya Ilolangulu wilayani Mbogwe kwa tuhuma za kumuua mke wake, Ester Joseph, kwa kumpiga na kitu kizito kichwani na kufariki dunia papo hapo.

Kamanda Mwaibambe alisema tukio hilo lilitokea Januari 28, mwaka huu huko katika Kijiji cha Bugomba na mtuhumiwa huyo alikamatwa na kufikishwa Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza na kesi yake inasubiri kikao cha Mahakama Kuu ili ianze kusikilizwa.

Kamanda Mwaibambe aliwataka wazazi na walezi kutoruhusu watoto kwenda kuwatembelea babu zao wenyewe ili kuondokana na vitendo vya ubakaji kama inavyodaiwa kutokea kwa mzee huyo wa miaka 89. Aliwataka wananchi wa Mkoa wa Geita kuacha tabia za kujichukulia sheria mkononi badala yake watoe taarifa katika vituo vya polisi vilivyo karibu ili kunusuru vifo vinavyotokana na wivu wa mapenzi.

# Muhimbili yawasha vifaa vya usikivu

**Na Mary Geofrey**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) imewasha vifaa vya kusaidia kusikia vinavyofahamika kwa jina la (Cochlear implant) kwa watoto saba wenye tatizo la usikivu.

Mkurugenzi wa Huduma za Upasuaji wa MNH, Dk. Sufiani Baruani, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa MNH, Prof. Lawrence Museru jana, alisema vifaa hivyo vinawasaidia watoto wasiokuwa na uwezo wa kusikia kwa asilimia 100.

Alibainisha kuwa kiwango cha madaktari wa ndani kufanya upasuaji wenyewe kimefikia asilimia 90 tofauti na awali walikuwa wakishirikiana na wataalamu wa nje ya nchi.

"Baada ya upasuaji, watoto hawa husubiri kipindi cha mwezi mzima ili waweze kuwashiwa vifaa husika. Katika kuwasha vifaa hivi leo, tulikuwa tukitegemea pia watalaamu kutoka nje, lakini kwa sasa tunafurahi kuwa eneo hili nalo tayari tumeliweza kwa asilimia 100 na leo tutafanya wenyewe bila kusaidiwa," alisema.

Dk. Buruani alisema kuwa tangu kuanza kutolewa kwa huduma hiyo nchini, jumla ya wagonjwa 49 wamefanyiwa upasuaji na kupandikizwa vifaa hivyo akiwamo mtu mzima mmoja.

Alisema kabla ya hapo walikuwa wakipelekwa nje ya nchi na mgonjwa mmoja ilimgharibu takribani Sh. milioni 100.

Alisema kwa kipindi cha miaka mitano walipeleka wagonjwa 50 na serikali iligharamia zaidi ya Sh. bilioni 4.6 lakini kwa wagonjwa 49 waliopatiwa matibabu nchini, wametumia Sh. bilioni 1.7.

Mkuu wa Idara ya Magonjwa ya Masikio, Pua na Koo wa MNH, Dk. Edwin Liyombo, alisema upasuaji unachukua saa tatu hadi nne kwa ajili ya kupandikiza kifaa ambacho atadumu nacho maisha yake yote.

Alisema mara baada ya kuwasha kifaa hicho cha kusikia, mtoto ataanza kusikia taratibu huku akiendelea kuhudhuria kliniki mara kwa mara hadi hapo atakaposikia vyema.

Alitaja sababu za watoto kupata tatizo hilo kuwa ni matumizi holela ya dawa wakati mama akiwa mjamzito, maambukizi ya homa ya uti ya mgongo na wengine wanapata matatizo wanapozaliwa endapo hatokatwa kitovu vizuri na kupata homa ya manjano.

Mtaalamu huyo alisema sababu zinazotokana na matatizo ya uzazi zimepungua na iliyobaki ni maambukizi ya magonjwa.

Alisema watu wazima wanapata tatizo kwa kukaa kwenye kelele zinazozidi kiwango kwa zaidi ya saa nane.

## HABARI KITAIFA




Mkuu wa Wilaya ya Kahama Festo Kiswaga akizungumza na vyombo vya habari mara baada ya kutembelea na kukagua ujenzi wa vyumba vya madarasa tisa vilivyojengwa kwa fedha za Uviko-19 zilizotolewa na serikali katika Shule ya Sekondari Mama Samia jana. **PICHA; SHABAN NJIA**

# Spika awaonya mawaziri

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amewataka mawaziri na manaibu wao kuhudhuria ipasavyo vikao vya Bunge kutokana na baadhi yao kusuasua kushiriki vikao hivyo.

Akizungumza juzi wakati wa kuahirisha shughuli za Bunge, Spika Tulia alisema: "Mnadhimu wa Serikali, mimi ninafahamu na ndiyo maana siku zote huwa ninasema hapa, hata mbunge akisema waziri simwoni, serikali ipo bungeni.

"Ni kweli serikali ipo bungeni lakini sote tunafahamu Waziri Mkuu ambaye ni mbunge lakini ni Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni lakini huwa anahudhuria bungeni na anakaa bungeni kusikiliza hoja za wabunge.

"Kama hakuonekana hapa, yupo kwenye kikao au amesafiri. Sasa wapo mawaziri, wapo Dodoma hayupo kwenye kikao lakini hayupo bungeni.

"Na pia wapo manaibu mawaziri wapo Dodoma, hawapo kwenye kikao lakini hayupo bungeni. Sasa tunakuwa tunalikosea heshima Bunge."

Dk. Tulia alisema wale ambao wapo kwenye kikao, Mnadhimu wa Serikali anatakiwa awe na taarifa nao.

"Kuna wale ambao hawapo kwenye kikao, hawajaitwa na Rais, Makamu wa Rais, wala Waziri Mkuu, wale ambao wanakuwa huko kote hawapo, wahakikishe wanakuwapo bungeni kwa sababu pamoja na kwamba wanapelekewa taarifa na utaratibu upo mzuri kabisa, ila lengo la serikali kuwa sehemu ya Bunge ni pamoja na wao kuwapo bungeni, wakati hoja za wabunge zikizungumzwa na wananchi ni vizuri mawaziri wakasikiliza wenyewe, " alisema.

Aliomba suala hilo lisisitizwe kwenye vikao vyao ili kuhudhuria ipasavyo vikao vya Bunge.

# Waziri Mkuu ataka kasi maandalizi sensa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amewataka wakuu wa mikoa yote nchini kuongeza kasi katika uratibu wa maandalizi ya sensa ya watu na makazi.

Majaliwa alitoa agizo hilo jana katika kikao kazi cha viongozi wa mikoa na wilaya kuhusu maendeleo ya maandalizi ya sensa ya watu na makazi itakayofanyika Agosti, mwaka huu.

"Twende kwa kasi ile ile ili jambo hili tulimalize kwa ufanisi mkubwa. Watanzania wanatuunga mkono na wanasubiri kwa hamu," alisema.

Akizungumza katika kikao hicho kilichofanyika kwa njia ya mtandao, Waziri Mkuu alisema kazi ya uwekaji wa anuani za makazi inatakiwa isimamiwe vizuri ili ikamilike kwa wakati.

"Zoezi (kazi) hili (hii) linatakiwa (inatakiwa) kutekelezwa kwa operesheni na kwa kipindi maalumu kama ilivyokuwa katika miradi iliyojengwa kupitia fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19," alisisitiza.

Waziri Mkuu alitumia fursa hiyo kuwapongeza wakuu wa mikoa na wilaya kwa kusimamia vizuri shughuli za serikali ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa ilani na maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Naye Kamisaa wa Sensa kwa Tanzania Bara, Spika Mstaafu Anna Makinda, alisema jambo hilo wanalitekeleza kwa ushirikiano na viongozi wa ngazi zote kuanzia mkoa hadi vijiji. Aliwashukuru viongozi hao na wananchi kwa ushirikiano wanaoutoa.

Kamisaa wa Sensa kwa upande wa Zanzibar, Balozi Mohamed Haji Hamza, alisema ameridhishwa na kazi kubwa ya sensa ya majaribio iliyofanywa mikoani na kusisitiza juhudi hizo ziendelee ili kuhakikisha malengo waliyojiwekea yanafikiwa. Kikao hicho kimehudhuriwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu,

Pindi Chana, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa.

Wengine ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, pamoja na maofisa mbalimbali wa serikali.

## Tahadhari yatolewa barabara Morogoro

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

BONDE la Wami/Ruvu limetoa tahadhari ya kuchukuliwa hatua za haraka kuondoa mchanga uliojaa katika Mto Magole ulioko Dumila mkoani Morogoro unaokatiza Barabara Kuu ya Morogoro-Dodoma kutokana na maji kukatiza juu ya daraja na kuhatarisha watumiaji wa barabara hiyo.

Kaimu Ofisa Maji Bonde la Wami/Ruvu, Elibariki Mmasi, alitoa hadhari hiyo jana baada ya kutembelea na kukagua mto huo ambao mara kwa mara umekumbwa na changamoto ya kufurika maji pindi mvua inaponyesha, hasa wilaya za Kiteto na Manyara.

Daraja linalokatiza mto huo lina historia ya kuzolewa na maji wakati wa serikali ya awamu ya nne na magari kushindwa kuvuka upande mmoja kwenda mwingine, hali iliyosababisha kujengwa usiku na mchana hadi kukamilika huku magari madogo yakilazimika kupitia Mikumi kutokea Kilosa hadi Dumila ili kuendelea na safari.

Kwa wiki mbili zilizopita, kwa nyakati tofauti, watumiaji wa barabara hiyo wamejikuta wakipoteza muda mwingi kusubiri maji kupungua katika Mto Magole ili waendelee na safari kutokana na maji kuwa mengi na kukatiza juu ya daraja.

Mmasi alitahadharisha kuwa kutokana na hali hiyo, ipo haja mchanga uliojaa ndani ya mto huo kuondolewa ili kuruhusu maji kukatiza chini ya daraja, vinginevyo kuna hatari ya hali kuwa mbaya zaidi kwa siku za usoni.

Kiongozi huyo alisema kunahitajika hatua za dharura wakati mamlaka zingine ikiwamo Wakala wa Barabara (TANROADS), Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Mazingira (NEMC) kuchukua hatua zaidi kunusuru daraja hilo.

Bonde la Wami/Ruvu limeendelea na upimaji wa ongezeko la maji katika mito inayokatisha barabara hiyo kutokana na mvua inayoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali.

HABARI KITAIFA



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Uchukuzi), Dk. Ally Possi, akitoa maelekezo kwa Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), Prof. Erick Massami, baada ya kukagua eneo la chuo hicho lililopo bandarini, wakati Naibu Katibu Mkuu huyo alipotembelea chuo hicho jijini Dar es Salaam. **PICHA: WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**

# Wakili: Uamuzi wa Sabaya, wenzake kutiwa hatiani kisha kufungwa sahihi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAKILI wa wajibu rufani katika kesi ya jinai namba 105, Veridiana Mlenza, amedai kwamba Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, ilifanya uamuzi sahihi wa kuwatia hatiani na kuwafunga miaka 30 jela aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai na wenzake wawili.

Pia wakili huyo alipinga madai ya hoja ya Wakili wa waleta rufani, Majura Magafu, kwamba polisi walipika vielelezo vya ushahidi ili kuwabambikia kesi wakati rufani na hakimu aliyekuwa akisikiliza shauri hilo kutokuchambua kwa kina ushahidi.

Wakili huyo alitoa madai hayo jana wakati wa usikilizwaji wa Rufani Na. 129 katika shauri lililokuwa linamkabili Ole Sabaya na wenzake wawili mbele ya Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Arusha, Sedekia Kisanya.

Akijibu hoja ya tatu za mawakili wa waleta rufani kwa nini wateja wao walistahili kutiwa hatiani na kufungwa miaka 30 jela, Wakili Mlenza alidai kwamba hakimu hakukosea kupokea kielelezo cha nne na cha tano.

"Kielelezo cha picha ya Bakari Msangi na fomu kutoka maabara ya uchunguzi wa kielektroniki "Forensic Beureu" kwamba zilipokewa kinyume cha sheria si kweli na hoja zao hazina msingi. Pia haki yao wamejinyima wenyewe kwa sababu wakati mahakama ya hakimu ikipokea kielelezo cha nne hawakusema kwamba vimepikwa," alidai.

Wakili huyo alidai kwamba waleta rufani wameshindwa kuthibitisha kwamba polisi waliokuwa wakichunguza shauri hilo walipika vielelezo na kuwabambikia kesi kwa kuwa walishindwa kuibua hoja za msingi wakati wa usikilizwaji wa kesi.

"Kuhusu nyaraka ya biashara na eneo husika la tukio lilipotokea ni hoja isiyo na mashiko kwa kuwa shahidi wa kwanza ambaye ni mmiliki wa duka, alifika mahakamani na kutoa ushahidi na maeneo wanayodai yametofautiana si kweli kwa kuwa ni eneo moja," alidai.

Pia Wakili huyo alidai kwamba si kweli hakimu alikataa hati ya utetezi wa kutokuwa katika eneo la tukio kwa washtakiwa kwa kifungu cha 194(4) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

"Hakimu alieleza kwamba mshtakiwa alitakiwa kumleta shahidi ambaye ni jirani yake kuthibitisha kwamba siku hiyo alikuwa nyumbani kwake. Alichokifanya hakimu ni sahihi," alidai.

Kadhalika alipinga madai ya waleta rufani kwamba hakukuwa na ushahidi unaoonyesha mshtakiwa wa kwanza na wa pili kukamatwa na kuhojiwa hakukuwa na mlalamikaji katika kosa la kwanza na tatu.

"Hoja hii haina mashiko kwa kuwa kama washtakiwa waliwekwa chini ya ulinzi na kufikishwa polisi, inaonyesha wazi kwamba walikamatwa na kuhojiwa na kwa mujibu wa shahidi wa kwanza wa mashtaka, alilalamika polisi kuchukuliwa Sh. milioni 2,769,000.

"Kuhusu kutokukamatwa kwa Sabaya na kuhojiwa kwa mujibu wa Inspekta Gwakisa, alidai kwamba alishindwa kumkamata kwa kuwa alikuwa na mamlaka ya uteuzi, hivyo ilitakiwa wapate kibali kutoka kwenye mamlaka ya uteuzi ndio sababu hawakumkamata," alisisitiza.

Kuhusu hoja ya upande wa mashtaka ya mashtaka kurekebisha hati ya mashtaka wakati shauri likiendelea mahakamani, wakili huyo alidai kwamba kifungu cha 234(1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinia kimetoa fursa ya kufanya marekebisho wakati kesi ikiendelea. Wakili mwingine wa wajibu rufani, Baraka Mgaya, akijibu hoja ya 13, alidai kwamba mahakama ya chini haikukosea kuwatia hatiani kwa kosa la unyanganyi kwa kuwa shahidi wa pili, tatu, nne, tano na sita wa mashtaka, walilalamika kuwa Sabaya alifanya unyang'anyi wa silaha akiwa na wenzake.

"Shahidi wa sita, Bakari Msangi, aliieleza mahakama kwamba aliombwa na Mohamed Saad kwamba aende dukani kwake kumsaidia kwa kuwa aliambiwa Sabaya yuko dukani humo. Alipofika alikamatwa, walimpekua na kuchukua Sh. 390,000, alipigwa, alifungwa pingu na kunyooshewa bastola kichwani na mrufani wa kwanza. Kwa mantiki hiyo, tukio hilo lilifanywa na zaidi ya watu wawili na mahakama ya chini ilikuwa sahihi kutoa hukumu hiyo. "Katika hoja yao ya tatu wanadai kwamba kitendo cha kuwapiga na kuwapekua watu dukani akiwamo Bakari Msangi, nia yao ilikuwa kumpata mmiliki wa duka Mohamed Saad, ni hoja isiyokuwa na msingi kwa kuwa walishiriki kutenda uhalifu huo katika eneo hilo.

"Ndani ya hoja yao ya tatu, mawakili wa waleta rufani wanadai kwamba kuna wahusika ambao hawapo mahakamani, lakini hakuna ubishi kwamba hata kama hawapo, lengo lao lilikuwa moja, hivyo si kigezo cha wao kutokushtakiwa na kutiwa hatiani," alidai Mgaya.

Akijibu hoja za tano, sita, tisa na 12, alidai kwamba malalamiko yao kwamba mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha ilishindwa kuthibitisha kama kosa la unyang'anyi wa kutumia silaha lilifanyika, si kweli kwa kuwa kuna kosa kama hilo lilitendeka na ni kwa mujibu wa kifungu cha 300 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

"Tukirejea makosa walioshtakiwa nayo, inatakiwa silaha iwe imetumika kabla na baada na katika mazingira hayo ushahidi unaweza kuthibitisha makosa hayo na yanaendana. Kosa hili linaweza kufanywa na mtu mmoja lakini wakiwa zaidi ya wawili inakuwa unyang'anyi wa kutumia nguvu ya silaha kwa mujibu wa kifungu 285(2) cha Sheria ya Unyanganyi wa Kutumia Kundi.

"Kwa kuwa kosa lilifanywa na watu zaidi ya wawili, ni sahihi kwa hakimu kutoa kosa la kwanza na tatu la unyang'anyi wa kutumia silaha kwenda katika kosa la unyang'anyi wa kutumia kundi," alidai.

Mgaya alidai kwamba kosa la unyang'anyi wa kutumia kundi lazima wizi uwe umefanyika kwa watu zaidi ya wawili na Februari 9, 2021 alikwenda mahakamani shahidi wa kwanza mmiliki wa duka na shahidi wa pili na alidai kwamba Sabaya alitoa amri apigwe na kupekuliwa na kuchukuliwa fedha taslimu Sh. 2,769,0000.

Kuhusu tukio la unyang'anyi wa kutumia silaha, alidai kwamba Februari 9, 2021, Sabaya akiwa eneo la tukio, alitoa amri shahidi wa sita, Bakari Msangi, kupigwa, kuwekwa chini ya ulinzi, kufungwa pingu na kupekuliwa kisha kuchukuliwa Sh.390,000. Pia alidai kuwa wakati mambo hayo yakiendelea, kulikuwa na matumizi ya silaha ambayo ilitumika kukamilisha kosa hilo.

Aidha, Wakili Mlenzi akijibu hoja ya kwanza, alidai kwamba hati ya mashtaka si batili kama ilivyodaiwa na waleta rufani kwa kuwa iliandaliwa kama sheria inavyoelekeza kwenye mashtaka hayo.

Alidai kwamba kwa kuwa mali zilizoibwa katika kesi hiyo zilitoka kwa watu tofauti, wasingeweza kujumuisha mashtaka yote kuwa pamoja kwa kuwa vitu vilichukuliwa kwa walalamikaji tofauti.

Baada ya kujibu hoja hizo, Jaji Kisanya aliahirisha usikilizwaji wa rufani hiyo hadi Februari 21 saa 3:00 asubuhi, kesi hiyo itakapoendelea tena.

# Padri awapa neno wanaodai kuponya wagonjwa kiroho

**Na Christina Haule,** MOROGORO

PAROKO wa Kanisa Katoliki la Mtakatifu Alois Gonzaga, Parokia ya Mvomero mkoani hapa, Padri Herman Kiangazi, amewataka viongozi wa dini wanaotangaza uponyaji kwa watu wenye ulemavu, kuwaponya kiroho na kimwili kwa kuzingatia uhitaji ikiwamo matibabu hospitalini.

Padri Kiangazi alisema hayo juzi kwenye tamasha la watu wenye ulemavu linalofanyika kila mwaka Februari duniani kwa ufadhili wa Tim Tebow, Mmarekani aliyejitolea kuwaenzi watu hao baada ya kuona jamii inawasahau.

Alisema pamoja na uponyaji wa kiroho, viongozi hao wanapaswa kuwapa ushirikiano wa hali na mali kama waamini ikiwamo kuwapa ushauri na kuwasaidia kupata huduma mbalimbali muhimu kupitia jamii inayowazunguka.

"Viongozi wa kiroho kama tulivyoguswa kwenye uponyaji, basi tuguswe na kuwasaidia kimwili kwa sababu pengine unayemwombea anahitaji huduma ya kitaalamu ikiwamo matibabu. Huenda ana upungufu wa damu au maji mwilini, hivyo tunapaswa kuwajibika kumsaidia pia ndipo huduma yetu ya kiroho itafanya kazi vizuri," alisema.

Pia aliwataka viongozi wenzake wa kiroho kuwapa kipaumbele watu wenye ulemavu kwa kuonyesha kuwajali na kuwathamini na ndipo wengine washiriki kuwa pamoja kwa kuwapa mahitaji muhimu ya mwili kama chakula, malazi na mavazi.

Aliwasisitiza viongozi wa kiroho kutambua kuwa wanapaswa kufungua njia ya upendo kwa watu hao sambamba na kutetea haki zao na kwamba kujiweka pembeni na kuwaacha kutafanya hata jamii inayowazunguka kuwatenga kwa kuwaona hawana umuhimu kwao.

Ofisa Ustawi wa Watu Wenye Ulemavu, ambaye pia ni mwanzilishi wa Kituo cha Kusaidia Watu Wenye Ulemavu wa Akili na Viungo (EMFERD) ambao ndio waandaaji wa tamasha hilo, Josephine Bakhita, alizisisitiza familia na jamii kuweka mbele upendo kwa watu wenye ulemavu. Alisema suala hilo linaonekana kupungua sana kwa watu hao na kuwakosesha amani ya moyo.

Alisema mhitaji amekuwa akikosa upendo popote anapokuwa hasa watu wenye ulemavu wa akili ambao ni kundi mojawapo linalotengwa na kuminywa katika jamii.

Bakhita alisema kila dhana nyeti ikiwemo haki za wenye ulemavu, zisimamiwe katika mambo muhimu ikiwamo kuwapatia huduma za afya na chakula jambo litakalosaidia kuondoa mauaji ya kimya kimya yanayowakumba watu hao kwa sasa.

Alisema kama kampeni zingine zinazopewa kipambele na msisitizo mkubwa kama ilivyokuwa kwenye chanjo ya UVICO-19, kundi hilo pia lifanyiwe kampeni kuanzia ngazi ya familia kwa kuwekewa hamasa hadi kwa watunga sera. Jambo hilo, alisema litasaidia jamii, nchi au duniani kutambua kuwa kundi hilo nalo linahitaji kuthaminiwa, kupendwa na kupewa matumaini ili nao wajiamini.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Dua njema kwa Simba wawakilishi pekee CAF

**WAWAKILISHI** pekee wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika ambayo yanaandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Simba wanatarajia kushuka dimbani ugenini kesho kupambana na wenyeji US Gendarmarie ya nchini Niger.

Simba au Wekundu wa Msimbazi kama inavyoitwa na mashabiki wake iko katika Kundi D pamoja na US Gendamarie, RS Berkane ya Morocco na Asec Mimosas kutoka Ivory Coast.

Mechi hiyo ya kesho itakuwa ni ya pili katika hatua ya makundi baada ya Jumapili iliyopita kuanza kwa ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Asec Mimosas, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

RS Berkane ndio vinara wa Kundi D baada ya wao kupata ushindi wa mabao 5-3 dhidi ya US Gendamarie na hivyo kesho atakayepata matokeo bora ndiye atakaa kileleni kwenye kundi hilo.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wanatakiwa kuingia katika mchezo huo kwa nidhamu ili wajiweke kwenye mazingira mazuri ya kusonga hatua inayofuata ya michuano hiyo ya pili kwa ukubwa barani Afrika kwenye ngazi ya klabu.

Kama wachezaji wa Simba wataendelea kujituma na kucheza katika kiwango bora kama walivyofanya kwenye mechi iliyopita dhidi ya Asec Mimosas, watakuwa kwenye nafasi nzuri ya kupata ushindi na hatimaye kuendelea kufukuzana na vinara wa kundi hilo, RS Berkane.

Tunawakumbusha wachezaji wa Simba kushuka dimbani wakifahamu wanapeperusha bendera ya Tanzania, hivyo wanatakiwa kuonyesha ubora wa juu.

Wakati wa kauli ya Kocha Mkuu wa Simba, Mhispania Pablo Franco kwamba kila mechi kwao ni sawa na fainali sasa inatakiwa ionekane kwa vitendo kwa sababu mechi za hatua ya makundi ni chache na kamwe isiwadharau wapinzani wao kwa kuangalia matokeo ya mchezo wao uliopita.

Ni wazi mashabiki, wanachama na wadau wa soka nchini bado hawajasahau matokeo ya kufungwa na kutolewa na Jwaneng Galaxy ya Botswana kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kwa kuamini timu hiyo ni ndogo au wamemaliza kazi, wachezaji wanatakiwa kuwa makini katika dakika zote 90 za mchezo.

Simba inatakiwa ifahamu si Watanzania tu wanawaangalia, lakini pia wanawawakilisha wananchi wote wa Afrika Mashariki kwa kuwa ni klabu pekee kwenye ukanda huu iliyobakia kwenye michuano hiyo.

Watanzania wanatakiwa kusahau tofauti na itikadi zao za ndani kwa kuiombea Simba ipate ushindi katika mechi ya kesho na itakapopata nafasi ya kusonga mbele, itakuwa imetoa nafasi kwa nchi kuwa na wawakilishi wanne katika mashindano yanayoandaliwa na CAF katika msimu ujao.

Kimsingi ni jambo gumu kwa wapinzani wao hasa Yanga kuwaombea dua njema, lakini moyoni wanafahamu matunda ambayo Tanzania itayapata endapo Simba itasonga mbele.

Tunafahamu gharama za maisha zimepanda, lakini kama kuna mashabiki wenye uwezo, huu ni wakati wa kusafiri pamoja na timu hiyo kwenda katika mechi zake za ugenini ili kuwaongezea hamasa wachezaji.

Kama ambavyo hufanya kwa timu zote zinazoshiriki mashindano ya kimataifa, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), lisichoke kukaa pamoja na viongozi wa Simba kuhakikisha kila kitu kinakwenda vizuri kwa sababu hata wao wanajua Simba ikipata matokeo chanya, sifa huwafikia wao kama wasimamizi wa mchezo huo hapa nchini.

Nipashe hatutaacha kutumia nafasi hii kuwakumbusha pia wachezaji wa Simba kucheza kwa nidhamu kwa sababu hata kama mchezaji ana uwezo lakini akikosa nidhamu, anaweza kuiweka timu yake kwenye hatari ya kupoteza pointi au yeye mwenyewe kujiondoa sokoni kwa wale mawakala wanaotafuta wachezaji.

Kila la kheri Simba, kila la kheri Tanzania katika michuano hiyo ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kosa amefanya mwamuzi, Karia anahusika vipi hapo?

Na Adam Fungamwango

**MJADALA** wa waamuzi nchini umeendelea kuwa mkali, na sasa Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, naye akiibuka na kulizungumzia hilo.

Alipokuwa akifunga semina ya waamuzi, Karia amewataka kushirikiana na kutimiza majukumu yao ya uwanjani kwa pamoja kwa sababu wao ndiyo wamesababisha kilio cha kutaka kuletwa hapa nchini kifaa au mashine ya msaada iitwayo VAR.

Akashangazwa kuona waamuzi wako watatu mpaka wanne uwanjani, lakini kazi hiyo inaonekana anaachiwa mmoja tu ambaye ni mwamuzi wa kati.

"Kuna maamuzi mengine yanafanyika ambapo mwamuzi wa kati hajaona, je wengine watatu hawajaona, wakaambiana? Au wanachunguzana au wanataka mmoja aingie kwenye lawama peke yake?" Akawauliza na kuongeza.

"Mafunzo yanakuja wakati muafaka wakati ambapo kuna taharuki kuhusu uchezeshaji wenu. Baadhi ya makosa ni ya kibinadamu, mengine ya uzembe au makusudi, yanapofanyika mimi ndiyo mhanga na tangu nimekuwa kiongozi sijawahi kumfuata mwamuzi kutoa maelekezo zaidi ya kuwaambia wachezeshe kwa haki," alisema Karia wakati akifunga semina hiyo.

Hata hivyo Karia alisema waamuzi wanatakiwa kulindwa na wasiingizwe kwenye matatizo ambayo si ya kwao, ingawa anakiri kuna baadhi si waaminifu.

Hili limekuja, baada ya mjadala wa takribani wiki mbili za waamuzi kushtumiwa kwa kile kinachosemekana kuchezesha vibaya.

Baadhi ya viongozi wa serikali, wadau wa soka, watangazaji wa wachambuzi wameonekana kuingia kati na kusababisha mjadala mkubwa.

Hata hivyo kwa uzoefu wangu kwenye masuala ya michezo, ni kwamba mhemko huu umekuja baada ya timu moja kuonekana inabebwa na nyingine inaonewa. Kama zote zingenufaika na maamuzi mabaya ya waamuzi wala haya yasingekuwepo.

Simba na Yanga kwa miaka mingi zimekuwa zikinufaika mno na makosa yanayoitwa ya kibinadamu. Na tumekuwa tukiandika sana ni kwa nini makosa ya kibinadamu yanazinufaisha zaidi timu hizo kongwe? Sijawahi kuona au kusikia mihemko kama hii ya sasa, kwa sababu tu timu moja ni kama haikunufaika na makosa hayo kama wenzao.

Ifike wakati sasa waamuzi wanapokosea, basi kosa libaki kwa waamuzi na si Rais wa TFF kwa sababu hahusiki na lolote. Hahusiki kuendesha ligi, kupanga waamuzi au kuchezesha.

Baadhi ya wadau wa soka wamekuwa na lawama za jumla yanapotokea matatizo kama hayo. Wanakosea waamuzi, lawama kwa Karia. Anakosea mwamuzi wa kati, lawama kwa waamuzi wote. Hata anapokosea mwamuzi wa pembeni, bado lawama zinaenda kwa waamuzi wote.

Nadhani sasa kila mtu abebe kosa lake. Kama ni la mwamuzi wa kati liwe lake peke yake, na kama wa pembeni alaumiwe yeye tu.

Namuunga mkono Karia anaposema kunakosekana ushirikiano baina ya waamuzi kusaidiana na kuamua kitu kimoja. Ni kama wote wanamtegemea mwamuzi wa kati. Asipoona yeye basi. Wa pembeni wao hudhani kazi yao ni kuonyesha mpira unatoka, au kosa. Kuna wakati mchezaji anafanyiwa rafu pembeni, lakini hanyooshi kibendera hadi mwamuzi apulize kipenga. Unashangaa kazi yake ni nini? Amewekwa kule kwa kazi gani?

Hebu wawaige waamuzi wa Zanzibar waliochezesha mechi ya fainali ya Kombe la Mapinduzi Zanzibar, mwaka huu.

Mwamuzi hakuliona tukio la kipa, Mathias Kigonya wa Azam kumrukia mguu, Pape Sakho, lakini aliitwa na mwamuzi wa pembeni akaifanya kazi iliyomfanya kuwa pale. Akamwambia kipa amefanya kitendo hicho kwani alikishuhudia, hivyo kumsaidia mwamuzi wa kati kufanya uamuzi wa kuamuru pigo la penalti.

Mwamuzi wa kati alishaonyesha kuchanganyikiwa, kwani hakujua nini afanye, maana hajaona tukio, lakini uwajibikaji wa pamoja ukafanya kazi. Waamuzi wa Tanzania Bara wanakwama wapi?

## HABARI BUNGENI



Mbunge wa viti maalumu, Nusrati Hanje akiuliza swali la nyongeza Bungeni jana Jijini Dodoma ambapo aliuliza serikali ina mpango gani kuipandisha shule ya sekondari Sepuka kuwa na kidato cha tano na sita. **PICHA IBBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yaanika vikwazo katika mikopo elimu ya juu

SERIKALI imetaja vikwazo kadhaa katika kukuza na kuendeleza Mfuko wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ikiwamo baadhi ya wanufaika wa mikopo iliyoiva kutojitokeza na kurejesha kwa hiari mara baada ya kumaliza masomo.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ilibainisha hayo jana bungeni katika majibu ya swali la Mbunge wa Lupembe (CCM), Edwin Swalle.

Mbunge huyo alitaka kujua kero zilizopo tangu kuanzishwa kwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB)katika kukuza na kuendeleza Mfuko wa Elimu wa Bodi ya Mikopo ili kukopesha wanafunzi wengi zaidi.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilibainishwa kuwa kikwazo kingine ni baadhi ya waajiri kutowasilisha kwa wakati orodha ya waajiriwa wapya ambao ni wanufaika wa mikopo na wengine kuchelewa kuwasilisha makato ya fedha kutoka kwa wanufaika ambao ni waajiriwa wao.

Ilisema kutokana na hali hiyo, serikali imeendelea kutoa elimu kwa wanufaika na waajiri ili kuhamasisha urejeshaji wa mikopo kwa hiari na kwa kuzingatia matakwa ya kisheria.

Vilevile, ilisema imeendelea kuimarisha ukaguzi kwa waajiri pamoja na kuwashirikisha wadau wa kimkakati kama Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kubaini wanufaika wapya na kuongeza kasi ya urejeshaji mikopo iliyoiva kwa lengo la kukuza na kuendeleza mfuko huo ili kukopesha wanafunzi wengi zaidi.

Wizara hiyo pia ilisema azma ya serikali ni kukuza na kuendeleza mfuko huo ili kukopesha wanafunzi wengi zaidi ambapo imekuwa ikiongeza fedha za bajeti ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kila mwaka.

Wizara hiyo ilitoa mfano kuwa katika mwaka huu wa fedha (2021/22), serikali imetoa Sh. bilioni 570 kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ikiwa ni ongezeko la Sh. bilioni 106 kutoka Sh. bilioni 464 za mwaka 2020/21.

# Ukitaka kuwafuga wanyapori nchini fuata utaratibu huu

WIZARA ya Maliasili na Utalii imeweka bayana namna inavyodhibiti usafirishaji wanyamapori nje ya nchi huku ikieleza taratibu za watu wanaotaka kuwafuga.

Wizara hiyo ilibainisha hayo jana bungeni ilipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalumu (CCM), Angelina Malembeka, aliyesema kuna fursa zimetolewa kwa watu binafsi kuanzisha ranchi, mashamba na bustani za wanyamapori.

"Je, ni wanyama wa aina gani wanaruhusiwa kufugwa na utaratibu gani unaotumika kuwapata na serikali ina mkakati gani kuhakikisha wanyama hao hawasafirishwi kwenda nje ya nchi?" Angelina alihoji.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema ufugaji wanyamapori katika ranchi, mashamba na bustani za wanyamapori unasimamiwa na Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009 na Kanuni za Usimamizi wa Maeneo ya Ufugaji Wanyamapori za Mwaka 2020.

Ilibainisha kuwa kwa yeyote anayehitaji kufuga, atapaswa kuwa na leseni inayotolewa na Kamishna wa Uhifadhi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) kwa kufuata vigezo vilivyowekwa.

Ilisema wanyamapori aina zote wanaruhusiwa kufugwa kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa, mfano aina ya mnyamapori, ukubwa wa eneo na upatikanaji wa chakula na bei zake zimeainishwa katika jedwali la sita la Kanuni za Usimamizi wa Maeneo ya Ufugaji Wanyamapori za Mwaka 2020.

Ilieleza kuwa kutokana na tamko la serikali lililotolewa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 25/5/2016 kuhusu zuio la biashara ya usafirishaji wa wanyamapori hai nje ya nchi, leseni zote zinazohusu usafirishaji wa wanyamapori hai nje ya nchi zilizuiliwa.

Ilisema ulinzi katika malango ya kutokea ikiwa ni pamoja na viwanja vya ndege, bandari, barabara na mipaka ya nchi umeimarishwa ili kuhakikisha hakuna wanyamapori au nyara inayosafirishwa bila kibali au leseni.

# Makato mishahara walimu yaibua hoja

MBUNGE wa Singida Mjini (CCM), Mussa Sima, ametaka serikali kutoa mwongozo wa Vyama vya Wafanyakazi hasa Chama cha Walimu Tanzania (CCM) kupunguza ada ya uanachama au kuweka mfumo utakaokubaliwa na wanachama wenyewe.

Akiuliza swali bungeni jana, mbunge huyo alihoji mpango wa serikali kuhusu suala hilo na kushauri kuondoa kabisa mfumo wa asilimia ili kuweka kiwango kitakachokubalika na wanachama.

Ofisi ya Waziri Mkuu ikijibu swali hilo, ilisema Vyama vya Wafanyakazi, ikiwamo CWT, vimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini Na. 6 ya Mwaka 2004 ambayo ndiyo inayoongoza vyama vya wafanyakazi, vyama vya waajiri na mashirikisho vikiwa na lengo la kusimamia haki na maslahi ya wanachama wake ambao ni wafanyakazi walio katika Sekta ya Elimu.

Ilisema kwa mujibu wa kifungu 47(c) cha sheria hiyo, kuwa sharti ni kwamba katiba za vyama lazima, zieleze kuhusu ada ya uanachama au njia yoyote ya kuamua ada hiyo.

Kwa mantiki hiyo, ilisema chama kupitia katiba yake na wanachama ndiyo wenye mamlaka ya kujadili na kukubaliana masuala ya ada za uanachama katika chama husika na siyo serikali.

Pia ilisema katiba ya CWT kupitia kifungu namba 23.1(c), imetoa mamlaka kwa mkutano mkuu kufanya mabadiliko ya katiba kwa uamuzi wa theluthi mbili za wajumbe walio na haki ya kupiga kura.

Ilisema mkutano huo wa wanachama ndiyo ulioamua kuhusu njia ya ukataji wa ada kwa asilimia mbili na hivyo kwa kutumia chombo hicho hicho, wanachama wanaweza kuamua kuweka utaratibu mwingine wa ukataji wa ada husika bila kuvunja sheria.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA




Ofisa Kitengo cha Kadi Benki ya NMB, Lightness Zablon, akizungumza wakati wa kuchezesha droo ya saba ya Kampeni ya 'NMB Mastabata Kivyako Vyako' iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Ofisa Huduma kwa Wateja, Suzan Manga na kushoto ni Msimamizi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), Elibariki Sengasenga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Bunge lapiga marufuku matumizi 'fedha mbichi'

**Na Salome Kitomari,**
DODOMA

BUNGE limesema ni marufuku kwa halmashauri nchini kutumia fedha mbichi, huku likitaka kuchukuliwa hatua kali kwa watendaji watakaobainika kutokutii agizo hilo.

Agizo hilo lilitolewa juzi bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Grace Tendegu, alipowasilisha taarifa ya mwaka 2020/21.

Alisema pendekezo hilo linakusudia kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika kukusanya na kutumia fedha za umma.

Mwenyekiti huyo alisema matumizi ya fedha mbichi yanalenga kukwepa kubainika kwenye mifumo ya kielektroniki ya mapato na matumizi, hivyo wahusika kujipatia fedha kiujanja.

Alifafanua kuwa fedha mbichi ni mapato yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa benki kwa kuwa utaratibu uliowekwa na serikali kuu unataka kutumia mifumo ya LGRCIS na EPICOR/MUSE kwa ajili ya kurekodi na kudhibiti mapato na matumizi.

Alisema taarifa zinazotokana na mifumo hiyo husaidia kuandaa hesabu jumuifu za halmashauri husika mwishoni mwa mwaka wa fedha.

"Fedha zinapotumika kabla ya kupelekwa benki (fedha mbichi) zinakuwa hazijarekodiwa kama zilikusanywa na kutumika mwishoni mwa mwaka husika wa fedha," alisema.

Tendegu alirejelea taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), iliyoonyesha jumla ya Sh. bilioni 18.769 zilizokusanywa katika halmashauri mbalimbali zilitumika kabla ya kupelekwa benki katika mwaka wa fedha 2019/20.

Alizitaja halmashauri hizo na kiasi kwenye mabano ni Wilaya ya Kaliua (Sh. milioni 183.2), Uyui (Sh. milioni 383.4), Manispaa ya Temeke (Sh. milioni 344), Siha (Sh. milioni 112.5), Itilima (Sh. milioni 54.9) na Chalinze (Sh. milioni 25.2).

**KUFUTWA MIAMALA**

Mwenyekiti huyo alisema walibaini kuna ujanja unaofanyika katika mifumo ya kielektroniki kwa kufuta miamala, jambo linalokwenda kinyume cha nia ya kuweka ufanisi katika kukusanya mapato.

"Tunapendekeza serikali ihakikishe mamlaka ya kurekebisha ama kufuta miamala kwenye mfumo wa mapato inabaki kwa Ofisa Masuuli (Mkurugenzi wa Halmashauri) tu baada ya kujiridhisha na nyaraka halisi za mapendekezo ya kufanya hivyo," alisema.

"Katika mwaka wa fedha 2019/20, jumla ya Sh. bilioni 4.5 zilifutwa kwenye mfumo kwa utaratibu huu ambao kamati haikubali," alisema.

Alizitaja baadhi ya hamashauri na kiasi kwenye mabano ni Wilaya ya Tunduru (Sh. bilioni 1.2), Wilaya ya Siha (Sh. milioni 624.2), Wilaya ya Nanyumbu (Sh. milioni 497.9), Wilaya ya Kilindi (Sh. milioni 320) na Wilaya ya Liwale (Sh. milioni 258.7).

# Mashine za kamari zateketezwa kisheria

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

BODI ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania imeteketeza mashine 33 ya michezo hiyo kutokana na kukiuka sheria na ukwepaji wa kulipa kodi ya serikali.

Mashine hizo za michezo ya kubahatisha zilikamatwa katika oparesheni iliyoendeshwa na bodi hiyo katika Manispaa ya Shinyanga Januari mwaka huu, zikiwa na thamani ya Sh. milioni 70.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, James Mbalwe, akizungumza jana na waandishi wa habari mjini hapa, alisema wamekamata mashine hizo kutokana na kukiuka taratibu za uendeshaji wa michezo hiyo.

Alisema mashine hizo 33 ambazo wamezikamata ndani ya mwezi huo katika Manispaa ya Shinyanga, zimeikosesha serikali mapato ya Sh. milioni 3.6.

"Baada ya kuzikamata mashine hizi, wamiliki wake walikimbia na kuzitelekeza na tulipozifungua ndani tumekuta zina kiasi cha fedha Sh. milioni 1.6 ambazo tunazitaifisha," alisema Mbalwe.

Aliongeza kuwa kwa mujibu wa sheria, mara baada ya kuzikamata mashine hizo, wanapaswa kuziteketeza kwa moto na ndicho ambacho wamekifanya ili kutoa fundisho kwa watu wengine ambao wanaendesha michezo hiyo kinyume cha sheria.

Alitoa onyo kwa wanaoendesha michezo hiyo ya kubahatisha, kuwa ni marufuku kuruhusu watoto kuicheza wala kuiweka karibu na maeneo ya shuleni na hospitalini.

## Ziara ya Samia Ufaransa yajibu

**Na Faustine Feliciane**

ZIARA ya Rais wa Tanzania Samia Suluhu Hassan Ufaransa imeanza kuzaa matunda ambapo msafara wa wafanyabiashara kutoka nchi hiyo ya Ulaya unatarajiwa kuwasili nchini mwezi ujao kwa ajili ya kutafuta fursa za uwekezaji kwenye sekta mbalimbali.

Rais Samia akiwa Ufaransa, pamoja na mambo mengine, alikutana na wafanyabiashara wa nchini humo ambao walionyesha nia ya kuja kuwekeza nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Balozi wa Ufaransa nchini, Nabil Hajlaoui, alisema msafara huo wa wafanyabiasha ni matokeo chanya ya mkutano wa Rais Samia na wafanyabiashara hao Ufaransa.

"Rais Samia akiwa Ufaransa alikutana na wafanyabiashara, aliwahakikishia mazingira mazuri ya kufanya biashara na kuwekeza hapa Tanzania.

"Na sisi kama nchi tumeona hili na kuwathibitishia, kundi la wafanyabiashara wataanza kuingia nchini mwezi ujao na watakutana na mamlaka husika za Tanzania," alisema Balozi Nabil.

Alisema Ufaransa itaendelea kushirikiana na Tanzania na nchi hiyo ya Ulaya imepanga kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara kwa Ukanda wa Afrika Mashariki.

"Ziara ya Rais Samia imeleta mabadiliko makubwa ya kiushirikiano, Ufaransa tunatambua jitihada za Serikali ya Tanzania na tumekubaliana maeneo mbalimbali ya ushirikiano," alisema Balozi Nabil.

Alisema ushirikiano ulioimarishwa kati ya nchi hizo mbili unatarajiwa kuleta manufaa kwa nchi zote mbili.

Pia aliainisha maeneo ambayo nchi hizo zimekubaliana kushirikiana kuwa ni ulinzi na usalama, uchumi wa bluu, miundombinu pamoja na mradi wa mabasi ya mwendokasi (BRT).

Katika makubaliano ya msaada, Balozi Nabil alisema ipo mikataba waliyokubaliana, akitaja baadhi ya msaada hiyo kuwa ni ya mikopo yenye riba nafuu.

Rais Samia alifanya ziara ya kikazi Ufaransa Februari 10 na kuhudhuria mkutano wa ngazi ya juu wa masuala ya bahari ambapo alishuhudia utiaji saini mikataba sita baina ya nchi hizo.





## Wakosa sifa za elimu ya ufundi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BARAZA la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) limesema wanafunzi 2,854 walibainika kuwa hawakuwa na sifa ya kusoma programu mbalimbali katika vyuo vya kati na vya ufundi katika mwaka wa masomo 2020/2021.

Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Dk. Adolf Rutayuga, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufungua kikao cha siku mbili na wawakilishi wa vyuo vikuu na maofisa wanaoshughulikia udahili katika vyuo vikuu nchini.

Dk. Rutayuga alisema baraza limekuwa na udhibiti wa udahili kwa vyuo ambavyo vimekuwa vikiwadanganya wanafunzi ambao hawana sifa ya kuwa na alama D katika masomo manne. Pia alisema kutokana na jitihada mbalimbali ambazo wamekuwa wakizifanya, walibaini wanafunzi 2,854 ambao hawakuwa na sifa ya kusoma Programu mbalimbali katika vyuo vikuu nchini katika mwaka wa masomo 2020/21.

"Kuna wanafunzi 2,854 ambao waligundulika kwamba hawakuwa na sifa ya kusoma programu mbalimbali ambazo vyuo vikuu vilikuwa vimewasilisha majina yao.

"Kama Baraza tusingekuwa na udhibiti wa udahili inamaana hawa wanafunzi walikuwa wanapotezewa muda wao kwa hiyo tuliviarifu vyuo na tukawambia mmewadanganya ambapo muongozo wa udahili unaeleza lazima wawe na sifa gani,"alisisitiza.

Kadhalika alisema lengo la kikao hicho ni kujadiliana changamoto mbalimbali ambazo zinajitokeza katika masuala ya udahili nchini.

"Tunautaratibu wa kukaa na wadau wetu kuhusiana na udahili na changamoto zipi zimepatikana ili kuweza kuzitatua kwa sababu ya wingi wa vyuo tutakutana nao kwa siku mbili hapa,"alisema

Pia alisema changamoto kubwa ambayo wanaiona ni iwapo miongozo ya udahili haitafuatwa hutokea matatizo makubwa kwa wanafunzi kwani hutumia muda mrefu kuwa chuoni huku wakiwa hawana sifa.

"Kikubwa ambacho tunakiona ni kama miongozo ya udahili haitafuatwa ni matatizo makubwa sana tutawasababishia wadau wetu ambao ni wanafunzi wanaosoma Programu hizo pamoja na wazazi wao na jamaa zao wanao walipia ada kwa kusoma vyuo ambavyo havijasajiliwa.

"Vyuo vinavyofanya hivyo havifanyi jambo zuri mwingine anasoma miaka mitatu halafu anaambiwa hatambuliki, tuna miongozo ya udahili ambayo inaeleza kila chuo kimesajiliwa kwa namba fulani na kinatakiwa kutoa mikopo na sifa za kuingia katika programu hiyo, kila programu inasifa zake za kuingilia na angalau uwe una ufaulu wa alama D nne na zinaeleza kwenye masomo yapi," alisema.

# Wajadili maboresho kanuni, ada kulinda usalama katika biashara

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TUME ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) imefanya kikao cha pamoja na wadau mbalimbali kupitia mapendekezo ya kuboresha kanuni ya ada na tozo ili kurahisisha ufanyaji wa biashara na kulinda usalama wa wananchi na mazingira.

Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Sayansi,Teknolojia na Ubunifu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Alexander Mtawa, alisema kikao hicho cha pamoja kimehusisha wafanyabiashara, taasisi za serikali na wawakilishi kutoka wizara mbalimbali.

Dk. Mtawa alisema serikali imekuwa sehemu ya juhudi za mapendekezo ya maboresho ya kanuni za ada na tozo katika kurahisisha ufanyaji biashara hapa nchini wenye lengo la kuleta maendeleo kwa wananchi na kujenga usalama wa mazingira na kulinda soko la nje la bidhaa za Tanzania.

Akizungumza kwenye ufunguzi wa kikao hicho ambacho ni cha pili tangu ilipoanzishwa TAEC, alisema kuna changamoto nyingi ambazo zinahitaji kujadiliwa na kupatiwa ufumbuzi kupitia wadau hao na kuleta manufaa kwa jamii.

"Kikao hiki kina nia ya kuboresha kasoro zilizopo kwenye kanuni ya awali, kuongeza uwezo wa kulinda wananchi dhidi ya madhara ya mionzi katika usimamizi wa kazi mbalimbali za TAEC na kuboresha mazingira rahisi ya ufanyaji wa biashara nchini.

"Nimejulishwa kuwa yako maeneo ambayo tozo imeondolewa kabisa na maeneo mengine imeshuka kwa kiwango kikubwa mfano katika eneo la uagizaji wa bidhaa za mnyororo wa vyakula.

Kanuni zilizopendekezwa zimeondoa ada kwa wafanyabiashara wadogo na inapendekezwa kutotoza shehena yenye thamani ya mzigo isiyozidi Sh. millioni moja, hivyo vipimo vya vyakula vilivyoagizwa kutoka nje (uchambuzi wa radioactivity) vitatolewa bila malipo," alisema.

Pia alisema katika upelekaji wa bidhaa nje ya nchi, inapendekezwa kuondoa tozo kwa bidhaa zenye thamani ya mzigo isiyozidi Dola za Kimarekani 2,000 na kushusha kutoka asilimia 0.2 hadi asilimia 0.16 ya thamani ya mzigo na kutakuwa na ukomo wa malipo wa Sh. milioni mbili ili kurahisisha biashara na kuondoa vikwazo kwa wafanyabiashara wadogo.

Kadhalika, alisema marekebisho hayo pia yanalenga kuboresha sekta ya afya na mazingira ili kuepuka hatari ya mionzi ambayo imeshuhudiwa katika maeneo mengi duniani.




Diwani wa kata ya Chang'ombe Jiji la Dodoma Bakari Fundikira akichangia hoja ya kupitisha mapendekezo ya mpango wa bajeti ya mwaka wa fedha wa 2022/2023 katika kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika Jijini Dodoma juzi. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Jiji Dodoma kukusanya mapato bil. 101/-

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma inakadiria kukusanya na kutumia mapato ya Sh. bilioni 100.9 katika vyanzo vyake vya ndani ikiwamo serikali kuu na wahisani mbalimbali.

Akizungumza na madiwani wa Jiji la Dodoma kwenye kikao cha kupitisha mapendekezo ya mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/23, Mkurugenzi wa Jiji, Joseph Mafuru, alisema fedha hizo zitasaidia kwenye shughuli za maendeleo ya halmashauri.

Mafuru alisema halmashauri itahakikisha inakusanya mapato kutoka vyanzo na vituo vyote vinavyotumia mfumo wa kielektroniki ili kudhibiti upotevu na kuandaa kanzi data ya viwanja vyote vinavyozalishwa kwa kuvidhibiti utoaji, ulipaji na uendelezaji.

Alibainisha bajeti hiyo itafanya pia tathmini ya madeni yake ambayo halmashauri inadai ili kuongeza mapato na kuanzishwa kwa kampuni itakayosimamia miradi yote ya kimkakati ikiwamo ya Dodoma City, Council Investment Complex Low - Cost Housing, Soko Kuu la Job Ndugai, Kituo Kikuu cha Mabasi na Nala Lory Park.

Mkurugenzi huyo alisema makadirio hayo ya bajeti yalipendekezwa yatawezesha kukamilisha miradi inayoendelea kutekelezwa,kuchangia nguvu za wananchi inapobidi ikiwa ni pamoja na kuimarisha sekta za elimu, afya, kilimo, mifugo na uvuvi na utoaji wa huduma katika maeneo ya pembezoni.

"Mpango na mkakati wa Halmashauri ya Jiji ni kuhakikisha tunaboresha makao makuu ya nchi. Tunataka kumwandikia Katibu Mkuu TAMISEMI (tawaka za Mikoa na Serikali za Mitaa) barua ya kuomba fedha kwa ajili ukarabati wa barabara za zamani pamoja na uwekaji wa taa barabarani na kufunga kamera kwa lengo ya kuangalia usalama,"alisema.

Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe, aliwataka madiwani na watendaji kuhakikisha bajeti hiyo inafanya huduma mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

Aidha, aliwataka madiwani kwenda kusimamia ukusanyaji wa mapato kwa uaminifu ili bajeti iliyopitishwa ikamilishe miradi yake ya maendeleo na kiibua vyanzo vipya.





# Waonywa kutumia tiba zisizo rasmi

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WIZARA ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imewataka wananchi wanaokabiliwa na maradhi yasiyoambukiza kuacha kutumia tiba asili na za kienyeji ambazo zinaweza kusababisha athari zaidi za kiafya.

Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, alisema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akitoa ufafanuzi wa mikakati ya serikali katika kutoa tiba kwa maradhi yasiyoambukiza.

Imebainika kwamba maradhi hayo kwa Zanzibar, yamekuwa yakiongezeka kwa asilimia 3.7, hivyo kuwataka wananchi kutumia tiba rasmi.

Alisema wizara imechukua jukumu la kutoa matibabu kwa wagonjwa wa maradhi yasiyoambukiza yakiwamo kisukari na shinikizo la damu, hivyo hakuna sababu tena ya kutafuta tiba nyingine ambayo haiko rasmi.

Wizara yake, alisema tayari imetenga vituo vya afya 53 kwa ajili ya kutoa tiba kwa wagonjwa wanaosumbuliwa na maradhi yasiyoambukiza ambayo yamekuwa tatizo kubwa kwa wananchi.

Pia alibainisha kuwa kazi kubwa inayofanywa kwa sasa ni kuongeza wataalamu zaidi wakiwamo madaktari bingwa watakaofanya kazi kwa ajili ya kutoa tiba sahihi kwa wagonjwa.

"Mheshimiwa Spika, tunawaomba wagonjwa wanaosumbuliwa na maradhi ya kisukari kuhakikisha wanatumia tiba rasmi zinazotambuliwa zenye vipimo sahihi na kamwe msitumie dawa za miti shamba ambazo si rasmi," alisema.




Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Mazrui (wa pili kulia) na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Mohamed (katikati) wakiwa kwenye picha ya pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa DKT International Tanzania, Kelvin Hudson (kushoto) na mabalozi wa bidhaa za DKT, Tamia Tibs (wa pili kushoto) na Calisah Abduhamid (kulia ) wakati wa uzinduzi wa kampeni ya cycle for HIV 2022 yenye lengo la kuhamasisha vijana uelewa wa kujilinda na ugonjwa wa Ukimwi nchini, ambapo kutakuwa na shindano la kutambua bidhaa za kampuni hiyo na washindi kushiriki mbio za baiskeli mjini Zanzibar.

# Alama za barabarani kuwekwa shuleni, sokoni

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WIZARA ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imesema itaweka alama za barabarani katika maeneo yote yenye mikusanyiko na harakati nyingi za watu ikiwamo shule na masoko ili kuepusha matukio ya ajali.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa wizara hiyo, Rahma Kassim Ali, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jangombe Ali Abdulgulam Hussein, aliyetaka kujua lini wizara itaweka alama za barabarani katika maeneo ya shule ili kuepuka ajali za mara kwa mara.

Waziri alisema ni kweli yamekuwapo matukio ya ajali mara kwa mara katika maeneo hayo yenye harakati nyingi za mkusanyiko wa watu na kwamba baadhi ya maeneo hayana alama za barabarani au zingine zimefutika.

Alisema kazi kubwa inayofanywa na wizara kwa sasa ni kuyatambua maeneo hayo kwa kushirikiana na wananchi na viongozi wa maeneo husika ikiwemo uongozi wa shule.

Pia aliitaja mikakati hiyo ikiwemo kufanya kazi na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani pamoja na kuhirikiana na wahusika kwa ajili ya kuweka alama za barabarani ambazo zitasaidia kupunguza ajali.

"Mheshimiwa Spika nataka niwajulishe wananchi na jimbo la Jang'ombe kwamba wizara itahakikisha inaweka alama za barabarani kwa ajili ya kudhibiti matukio ya ajali ambazo husababisha vifo na majeruhi kwa wananchi wakiwamo wanafunzi wa shule," alisema.

Pia aliwataka wananchi kuacha tabia ya kung'oa miundombinu hususani alama za barabarani inayowekwa na serikali kwa ajili ya kudhibiti matukio ya ajali barabarani. Alisema baadhi ya miundombinu huibwa na wananchi kwa ajili ya matumizi ya vyuma chakavu , hivyo kuitia hasara serikali.

# Kamati yataka ujenzi Bandari Mangapwani

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

KAMATI ya Baraza la Wawakilishi ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati imeitaka Serikali kutafuta wawekezaji zaidi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya uchumi wa bluu katika ujenzi wa bandari ya Mangapwani, Kaskazini Unguja ambayo itasaidia kukuza uchumi na mapato.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Yahya Rashid Abdalla, alisema hayo wakati akiwasilisha ripoti ya kamati katika kikao cha Baraza la Wawakilishi kinachoendelea Chukwani, nje kidogo ya mji wa Zanzibar.

Alisema Zanzibar inahitaji bandari ya uhakika ambayo itakuwa na uwezo wa kupokea mizigo mbalimbali na bidhaa zikiwamo makontena kutokana na bandari iliyopo sasa kuwa na uwezo mdogo, hivyo kuzidiwa na mizigo.

Yahya alisema ujenzi wa bandari ya Mangapwani ni muhimu kwa kuwa itakuwa na uwezo mkubwa wa kuchukua mizigo mbalimbali ikiwamo huduma za mafuta na makontena.

"Mheshimiwa Spika kamati yetu inaiomba serikali kuendelea na mchakato wa kutafuta wawekezaji kwa ajili ya kutekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa bandari huko Mangapwani Mkoa wa Kaskazini Unguja ambapo juhudi zinaendelea hadi sasa," alisema.

Pia kwa niaba ya kamati hiyo, alisema juhudi za haraka zinatakiwa kuchukuliwa na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kwa ajili ya kulinda vyanzo vya maji ambavyo baadhi yake vipo katika hali mbaya ya uvamizi wa makazi ya watu.

Alisema vyanzo vingi vya maji vipo katika hali mbaya ya kutoweka kutokana na kuwepo kwa mabadiliko makubwa ya tabia ya nchi na kazi ya uvamizi.

Alizitaja juhudi ambazo zinatakiwa kuchukuliwa na ZAWA kuwa ni pamoja na kuzungusha uzio ambao utalinda vyanzo hivyo.

Wakichangia ripoti hiyo, Mwakilishi wa Kijitoupele, Ali Suleiman Mrembo, alishauri serikali kuwekeza katika Shirika la Nyumba ili lifanikiwe na kutekeleza majukumu yake.

Alisema Shirika la Nyumba limepewa majukumu makubwa lakini halina mtaji wa fedha ambao utawezesha kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
DANI
TELE
JUMAMOSI FEBRUARI 19, 2022



TOLANI WATU WA AINA HIYO WAPO WENGI Uk.14



## KISHINDO CHA SUGU

# Watu watarajie nini baada ya kurudi jukwaani?

BAADA ya kimya cha miaka sita, hatimaye rapa mkongwe, Joseph Mbilinyi, maarufu kama ' Sugu', amerejea kwa kishindo katika tasnia ya muziki.

Sugu ambaye alikaa pembeni kwa muda kutokana na kutingwa na majukumu ya ubunge, ametambulisha ngoma yake mpya inayoitwa 'Taita' ambayo amemshirikisha Billnass

Akizungumza na BT, amesema alikuwa kimya kutokana na kutingwa na majukumu ya kijamii, lakini sasa anajiona yuko huru baada ya kazi kupungua.

"Ninataka kufikia Mei niwe nina kama nyimbo tatu, kwani kipindi hicho nitakuwa ninasherehekea miaka 50 ya kuzaliwa, hivyo ninataka nifanye japo kitu kidogo kwa mashabiki wangu," alisema Sugu.

Amefafanua lengo lake ni kuendelea na shughuli za muziki na kurudisha jina lake kama ilivyokuwa nyuma.

"Muda mrefu mashabiki wangu wamekuwa wakiniomba nitoe nyimbo mpya, nami nimesikia maombi yao, lakini baada ya Mei ndipo nitaamua niendelee kutoa nyingine zaidi au hapana," alisema.

Sugu ameeleza huenda akatoa wimbo mwingine na ambayo itamshirikisha rapa machachari Ney wa Mitego, kwa kile alichosema msaani huyo anaimba nyimbo za kiharakati kama yeye.

Mwanamuziki huyo mkongwe ni miongoni mwa watu walioanzisha muziki wa Bongo Fleva na kujipatia umaarufu mkubwa na hata kumwezesha kujulikana kwa watu wengi kabla ya kuingia kwenye siasa na kufanikiwa kupata ubunge.

BASI SAWA

## Madee usimpe kichwa Mganga

MWANAMUZIKI mkongwe kutoka Manzese, Madee Seneda, amesema katika kizazi cha sasa hakuna mwandishi bora wa nyimbo za mapenzi kama Kassim Mganga.

Madee ambaye alikuwa akishuhudia Maganga akitumbuiza katika tamasha la Mahaba Ndi ndi ndi, amesema badala ya marehemu Issa Matona, msanii huyo ameziba nafasi yake vizuri.

"Moja kati ya waimbaji bora kabisa kuwahi kutokea kwenye ardhi ya nyumbani Tanga na nyumbani Tanzania, kwenye uandishi wa nyimbo za mapenzi ukimtoa Issa Matona hakuna kama Kassim Mganga".




## Genevieve ushauri wako unatosha

MSHINDI wa Miss Tanzani na mwimbaji wa Bongo Fleva, Genevieve, amesema kujichanganya katika sanaa unaweza kujipatia kipato kikubwa zaidi.

Amesema muziki ni sehemu ya kipaji chake, lakini amekuwa akiigiza katika tamthilia mbalimbali ambazo huko anapata pesa nyingi ambazo zinaweza kukidhi mahitaji yake.

"Unapochanganya sanaa kama mimi unaweza kupata kipato kikubwa kutokana na kutoegemea sehemu moja. Ninafanya vizuri katika uigizaji kiasi ambacho napata pesa nyingi kwa kazi hiyo," amesema Genevieve.





## Wolper umekereka sasa wachambe

KUNA jambo limemkwaza staa wa filamu Bongo Jacqueline Wolper, na sasa ameamua kufunguka ili watu wenye tabia hizo waziache.

Kupitia Snapchat, Wolper, amesema kuna baadhi ya watu hawana tabia ya kumsifia mtu akiwa hai, badala yake wanasubiri afariki dunia.

"Hivi mtu ukifa kwanini unakuwa staa, yaani jamani mtu ungekuwa unapewa nafasi ya kuamka na kuona hao watu wamekuposti na kuandika kwa uchungu na kurudi kulala nahisi wengi wangeomba nafasi pia ya kuwapiga kwanza au kuwasuta, " ameandika.



## Irene Uwoya si mwenzenu tena

MSANII wa filamu wa Bongo Muvi, Irene Uwoya, anazidi kuwachanganya mastaa wenzake kutokana na aina ya bata analokula kila siku akifurahia maisha.

Baada ya kufanya starehe za aina yake huko Dubai, msanii huyo ameonekana mitandaoni akiwa na gari lake jipya aina ya Hummer ambalo ameweka kibao cha namba chenye jina lake.

Gari hilo ambalo limetengenezwa Marekani na linapendwa kutumiwa na mastaa mbalimbali duniani, inadaiwa uwoya atakuwa ametumia kiasi cha milioni 60 hadi 70, kama gharama ya kununua na kulisajili.

## Mangeshkar kinanda kilichowaburudisha wengi

**Na Adam Fungamwango**

LATA Mangeshkar inaweza ikawa ni jina geni miongoni mwa wasomaji na mashabiki wa muziki na filamu za Kihindi kwa Watanzania wengi.

Lakini nyimbo alizoimba na kutumiwa na mastaa wakubwa kwenye filamu mbalimbali, ni maarufu zaidi kuliko yeye mwenyewe hapa Bongo.

Dunia na ulimwengu wa mashabiki wa muziki na filamu za kihindi Februari 6, wamempoteza mmoja wa waimbaji mashuhuri wa muziki huo. Amefariki akiwa na umri wa miaka 93. Hadi anafariki alikuwa na afya yake nzuri na alikuwa bado anaimba nyimbo mbalimbali ambazo zinatumiwa kwenye filamu mbalimbali.

Alifariki kwa ugonjwa wa COVID-19 kwa mujibu wa taarifa kutoka nchini India.

Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi, aliwaongoza maelfu wa waombolezaji kwenye mazishi Jumamosi iliyopita ambayo yalikuwa ni ya kitaifa. Mastaa wa filamu maarufu kama Shakh Rukh Khan, Ranbir Kapoor, Aamir Khan na wengine wengi walihudhuria mazishi ya mwanamama huyo nguli, aliekuwa na sauti nyororo na ya kupendeza ambayo haikubadilika hadi anafariki.

Lata Mangeshkar ni mmoja wa wanamuziki waliowaimbia 'mastaa' wengi nchini humo na filamu zao zikapendwa sana hata hapa nchini. Si filamu tu, hata nyimbo zake, ziliigwa na baadhi ya makundi ya taarab na wanamuziki wake.

**MERE NASEEB MEIN-AMITABH BACHCHAN**

Lata aliimba wimbo 'Mere Naseen Mein', uliobeba jina la filamu ambayo staa wake ni Amitabh Bachchan iliyotoka mwaka 1980.

Wimbo huu uliigwa na Muungano Calture Troupe, mirindimo na kila kitu, kasoro maneno, wao wakaimba 'safiri salama swahiba mpenzi, upate neema uendako na enzi, ukumbuke nyuma, ninayo majonzi, urundi mapema unitoe simanzi.'

**KARISHMA YE KABHI DEKHA-TARZAN**

Kwenye filamu ya Tarzan, iliyotoka mwaka 1985, Lata, aliimba wimbo wa 'Karishma ye Kabhi Dekha na Hoga.' Kwa waliotazama filamu hii, wimbo huu unaimbwa sehemu ambayo Tarzan ameletwa mjini, na anapigwa mijeledi, akilazimishwa acheze michezo ya nguvu, akiwa juu, chini akiwa ametegewa nyaya zenye ncha kali. 'Demu' wa Tarzan alionekana kuimba wimbo huu wa huzuni akimuonea huruma mpenzi wake.

**ZINDAGI MAHEK-GOVINDA (HATYA)**

Hatya ni filamu ya mwaka 1988. Staa ni Govinda na mtoto wa miaka mitano wakati huo, Sujitha aliyecheza kama Raja akiwa ni bubu, Wabongo wakampachika jina la Yaya. 'Zindagi Mahek' ni moja ya wimbo ulio kwenye filamu hiyo nao pia uliimbwa na marehemu Latha Mangeshkar.


**ZU ZU ZU YASHODA-SAJOG**

Kwenye filamu ya 'Sanjog', iliyotoka mwaka 1995, marehemu aliimba wimbo uliotwao 'Zu zu zu Yashoda' ambao uliigwa na mwimbaji wa taarab Ally Star akiwa na TOT Plus mwanzoni mwa mwaka 2000, akauita 'Zuzu'. Akauimba 'Zuzu zuzu zuzu, siyo zuzu mie...'

**DIL TO PAGAL HAI-SHAH RUKH KHAN**

"Dil to Pagal Hai' ni moja ya wimbo maarufu sana kwa miaka ya hivi karibuni. Nao pia umeimbwa na Lata na mwimbaji wa kiume Udit Narayan. Umaarufu wake siyo tu kwa sababu ya filamu inayobeba wimbo huo iliyotoka mwaka 1997 ambayo imeechezwa na staa anayependwa kwa kizazi hiki Shah Rukh Khan, lakini pia sehemu ya maneno ya wimbo huo yaliimbwa na Isha Mashauzi kwenye wimbo 'Jeshi la Mtu Mmoja'.






## Azuka; Umbuko la Mfalme Juha

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI ni dhamama na mtu anayeupata inapaswa atumikie wananchi na si wananchi wamtumikie yeye. Kuna watu ambao wakipata mamlaka wanayatumia si tu kwa manufaa yao, bali hata kufanya mambo ambayo ni kinyume na maadili.

Wapo ambao wakipata uongozi, basi si tu huwa wala rushwa na kujilimbikizia mali, lakini pia kujihalalishia mpaka kuchukua wanawake ambao si wa kwao. Wanawachukua kinguvu bila kujali ana mtu wake au ameolewa haogopi kwa sababu ana madaraka.

Mtunzi wa filamu ya 'Azuka' ameona mbali sana kuandika hadithi hii ambayo itakuwa ni fundisho kwa watu waliopewa dhamana, wasivuke mipaka yao kwa sababu wanajua watalindwa na dola kutokana na uongozi wao. Ipo siku uongozi unakwisha na yote hayo analipwa.

Imechezwa na baadhi ya waigizaji ambao ni Mwadua Jawa ambaye ni mtunzi na akacheza kama mfalme, Hussein Al Eda na Hassan Al Eda, Bi Jasi, Salima Lema, Kibeku, Fatime Abdallah aliyecheza kama Azuka.

Kwenye himaya ya mfalme Kaiwanga, kuna binti mmoja mzuri ambaye ndiyo anaingia sasa kwenye usichana wake, Azuka. Ubichi na urembo wake unamzuzua mpaka mfalme. Anaamua kuwaambia walinzi wake wakamchukue na kumletea kule porini walikoenda. Anambaka na baada ya kumaliza humuonya kama akitoa siri hiyo, basi atauawa.

Siku ya ngoma kwenye himaya Vunde inafika, ambapo wasichana wote wanatakiwa kwenda kucheza ngoma. Azuka anashindwa kucheza, japo ni msichana mdogo, na cha ajabu zaidi akaanza kutapika. Uchunguzi ukaonyesha kuwa ni mjamzito. Habari inamfikia mfalme na kuamua akamatwe kwa siri na kutupwa kwenye msitu mnene akaliwe na wanyama. Walinzi wanatekeleza. Waliporudi kumpa habari kijana mmoja aitwaye Dovisa anasikia siri hiyo. Wanamshtukia, na yeye anakamatwa na kwenda kumtupa kwenye msitu huo.

Mizimu inawalinda kwa sababu hawana hatia. Mzimu unawatokea msituni na kuwaagiza kwenda kwenye himaya kueleza ukweli wote.

Ngoma inawaita wanahimaya wote bila mfalme kuwa na taarifa. Wakati mke wa mfalme anashangaa, Azuka na Dovisa wanatokea na kueleza ukweli wote. Mzimu wa msituni uliowalinda nao utajitokeza kuja kushindilia na kukazia hoja. Unawaadhibu walinzi, na mfalme mwenyewe kwa kuwaangamiza. Azuka mwenye ujauzito wa mfalme na Divisa wakaushikilia utawala wa mpito.



# Kim amtupia lawama Kanye

MWANAMITINDO na mshiriki wa kipindi cha maisha halisi cha televisheni, Kim Kardashian anadai kuwa na wasiwasi kuhusu mpenzi wake mpya, Pete Davidson, kwamba anaweza kuumizwa kutokana na maneno ya aliyekuwa mume wake Kanye West.

Kanye alituma ujumbe mfupi ambao alitumiwa na Kim, ambaye alilalamika maneno anayotoa kupitia mitandao ya kijamii yanamuweka katika mazingira ya hatari mpenzi wake huyo.

"Unaunda mazingira ya hatari na ya kutisha kiasi cha mtu anaweza kumuumiza Pete na hii yote itakuwa kosa lako," ujumbe huo umesema.



## Tolani watu wa aina hiyo wapo wengi

ALIYEKUWA Mshiriki wa Big Brother Naija (BBNaij) Tolani Baj , amesema baadhi ya mastaa nchini Nigeria wanaishi maisha feki ya kifahari.

Tolani amesema hayo kupitia ukurasa wake wa Snapchat, ambapo ameeleza kuna mastaa anawajua hawana maisha ambayo wanayaonyesha katika mitandao ya kijamii, badala yake wanaendeleza uongo.

"Namenda maisha ya kawaida, fikiria kuna watu wanaishi maisha mazuri lakini ni uongo kwani wana mawazo mengi kutokana na hali zao jinsi wanavyoishi," ameandika.


## Mama wa Burna Boy mcharuko

MAMA wa mwanamuziki wa Nigeria, Burna Boy, amezidi kuibua mjadala katika mitandao ya kijamii kutokana na vitendo vyake vya kushangaza.

Bose Ogulu, ambaye pia ni meneja wa mtoto wake, ana kawaida ya kupanda jukwaani kwa Burna Boy na kuanza kusakata vilivyo muzi.

Safari hii, amewaacha hoi mashabiki wa mwanamuziki huyo pale alipopanda jukwaani kucheza muziki pamoja na wachezaji wengine huku mwanawe akiwa nyuma akimwangalia.





## Trey Songz kwa nini lakini?

MWANAMUZIKI wa Marekani, Trey Songz anazidi kuandamwa na mikosi, baada ya mwanamke mmoja kujitokeza akidai kumlazimisha kufanya mapenzi kinyume na maumbile.

Kulingana na taarifa za mrembo huyo, Alias Jane Doe, amesema kabla ya tukio hilo yeye na Songz walikuwa na uhusiano wa kimapenzi tangu mwaka 2016.

Doe amesema Trey, alimualika katika sherehe iliyofanyika katika nyumba yake mjini Los Angeles, ndipo alipofanyiwa kitendo hicho bila ridhaa yake.

## Kylie, Travis wampa jina mtoto wao

MWANAMITINDO na mjasiriamali, Kylie Jenner na mume wake Travis, hatimaye wametaja jina la mtoto wake wa pili ambaye amezaliwa hivi karibuni.

Kylie aliandika katika ukurasa wake wa Instagram kwamba mtoto wao wa kiume anaitwa Wolf Webster, jina ambalo limependekezwa na wazazi wote wawili.

Travis na Kylie wamekuwa na uhusiano tata katika ndoa yao, mara kadhaa wameripotiwa kuvurugana na kutengana, lakini baada ya muda mfupi wanakuwa pamoja.



MAKALA

# Mwanamke anyofolewa figo na mwajiri wake

**Na Mwandishi Wetu**

## ●Alikwenda Saudia Arabia kufanya kazi za ndani



Judith Nakintu akionyesha jeraha lilotokana na upasuaji wa kuondoa figo aliofanyiwa wakati akiwa nchini Saudia Arabia akifanya kazi za ndani

HALI ya kutisha imemkabili mwanamke mmoja raia wa Uganda, baada ya kugundulika kunyofolewa figo na bosi wake, na kisha kumrejesha kwao akiwa taabani.

Imeelezwa vitendo hivyo vya kikatili vinawapata wanawake wengi wa Kiafrika wanaokwenda kufanya kazi za ndani katika nchi za Kiarabu.

Hata hivyo, kutokana na ukosefu wa ajira makundi ya wanawake yamekuwa yakimiminika katika nchi hizo kutafuta kazi kwa ajili ya kuhudumia familia zao ambazo nyingi ni masikini.

Katika tukio hilo ambalo limethibitishwa na madaktari wa nchini Uganda, imeelezwa mwanamke huyo Judith Nakintu (38), alikuwa akifanya kazi ya nyumbani nchini Saudi Arabia, aliondolewa figo yake ya kulia, kisha ilitolewa taarifa ya uongo kuwa alipata ajali ya gari.

Wizara ya Mambo ya Ndani imethibitisha hilo, baada ya kupewa ripoti ya uchunguzi kutoka Hospitali kuu ya kitaifa ya Mulago.

Kufuatia taarifa hiyo ya uchunguzi, sasa familia yake imeiomba serikali kuingilia kati kwa kusimamia suala hilo ili haki ipatikane kwa kukamatwa kwa tajiri au kulipwa fidia.

Judith ana watoto watano na alichukuliwa na kampuni ya Nile Treasure Gate mnamo mwaka 2019 kwa ajili ya kwenda kufanya kazi za ndani katika mji wa Jeddah nchini Saudi Arabia.

Baada ya kufanya kazi karibu miezi miwili, mawasiliano yake na familia yake yalikatika, ndipo mama yake mzazi alipoanza kufuatilia karibu miezi mitatu na alifanikiwa kupata taarifa kwamba mwanae amepata ajali.

'Tajiri wake alitufahamisha kwa simu kwamba mtoto wangu alipata ajali alitaka kufahamu familia yake, nikamuuliza alipata ajali bila kampuni iliyompeleka kujua?


Anasema kutokana na maelezo hayo aliamua kuwapigia simu kampuni yake na kuwaeleza mkasa wote, wao walimhakikishia hawana habari wala taarifa zozote.

Oktoba 30 mwaka jana, Kampuni hiyo ilimpigia mama wa Judith na kumtaarifu kwamba mwanawe alikuwa anatarajia kuwasili katika uwanja wa ndege wa Entebe siku hiyo.

Mama huyo alifika kwenye uwanja huo wa ndege kwa ajili ya kumpokea mwanae. Alipowasili alimuona mwanawe akiwa hajiwezi huku akiwa katika kiti cha wagonjwa.

Anasema kutoka ndani ya ndege alisaidiwa na wahudumu kwa sababu hakuweza kutembea na alipokamilisha taratibu aliingizwa kwenye gari la wagonjwa na kupelekwa Hospitali ya Mulago.

Kesho yake waliruhusiwa kwenda nyumbani, lakini ripoti ilionyesha alipata ajali ya gari jambo ambalo mama huyo akawa na wasiwasi nalo.



Judith Nakintu alivyo kwa sasa baada ya kuondolewa figo moja na mwajiri wake.

'Tulipolala hospitali maofisa wa kampuni waliyemchukua wakamleta daktari kufanya uchunguzi wa kitabibu, alipokamilisha waliniambia yupo sawa hana tatizo, lakini mimi sikuridhishwa, " anasema mama huyo kwa uchungu.

Hata hivyo siku ya Jumatatu alirudi katika hospitali hiyo kwa ajili ya kumfanyia tena uchunguzi, na safari hii aliambiwa taarifa ya kushtua kwamba mwanawe figo moja imetolewa.

Ofisa mratibu wa kuzuia ulanguzi wa binadamu kutoka Idara ya Uhamiaji Uganda, Agness Igoye, aliwaeleza waandishi wa habari kwamba, Hospitali ya Mulago imethibitisha kwamba mwanamke huyo alitolewa figo moja.

Uchunguzi huo umethibitisha figo yake ya kulia ilitolewa , na haraka Polisi walianza upelelezi na kumgundua mwajiri wake wa nchini Saudi Arabia, anayetambulika kwa jina la Sadaffa Muhamed.

Upelelezi huo umethibitisha ripoti iliyotolewa ilikuwa bandia na ililenga kuwadanganya wanafamilia ya muathiriwa. Katika ripoti ya awali ilionyesha sehemu zake zote za viungo zipo sawa wakati sio kweli.

Ripoti ya awali kutoka Polisi wa Saudi Arabia, ilionyesha Judith ambaye kwa sasa amepooza, alipata ajali akiwa kwa mwajiri wake.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa na mtandao wa Independent nchini Uganda, Kampuni ya Nile Treasurer, siku chache baadaye ilipokea taarifa kuwa watoto wawili wa waajiri hao wamefariki dunia kutokana na ajali hiyo, bahati nzuri Nakintu alinusurika ingawa ameumia sana na kusababisha damu yake kuganda.

Kwa upande wake, Rais wa Migrant Workers Voice, inayoshughulikia masuala ya wafanyakazi wahamiaji, Abdallah Kayonde, anasema ameiandikia Kampuni hiyo kulipa fidia ya shilingi milioni 600 za Uganda kwa kitendo cha kutolewa figo ya muathirika huyo kinyume cha sheria na kuuzwa.

**BBC**

### TULIKOTOKA, TULIKO & TUNAKOELEKEA...

# Matokeo ya mechi yalijulikana mapema saa mbili kasorobo

**Na Adam Fungamwango**



TEKNOLOJIA siyo tu kwamba imebadilisha dunia, lakini imerahisisha vitu vingi ambavyo wakati mwingine ukivifikiria unabaki kucheka peke yako.

Kwa wakati ule ilionekana ni sawa tu, lakini kwa sasa unabaki unajiuliza ni jinsi gani ambavyo uliweza kuishi kwenye hali ile. Ni kwa sababu tu haikujulikana kama inakuja siku ambayo dunia nzima itakuwa kiganjani.

Kumbuka enzi ambazo watu wanaandikiana barua. Mtu anamuandikia baba au mama yake barua kwenda kijijini. Anaipeleka kwenye kampuni moja ya basi na kumkabidhi konda au dereva. Tena enzi hizo hawakuhitaji hata pesa ya kulipia ubebaji, au usumbufu. Anaagizwa tu, ukifika sehemu fulani, hata gari lisisimame, aitupe tu hiyo barua.

Na kweli, kwa sababu ilikuwa imeandikwa jina la mtu fulani maarufu. Itagaragara hapo kando ya barabara hadi mtu mmoja aione, ataiokota na akisoma jina la mzee huyo itapelekwa moja kwa moja hadi kwake.

Naye ataifungua na kuisoma. Ataona aliyeandikiwa ni mzee fulani, kwa hiyo atafunga safari kwenda kumpelekea. Zamani watu walikuwa waaminifu na Wajamaa kweli kweli, hata kama ilikuwa na pesa, itafika bila hata ya kunyofolewa hata noti moja.

Nyingine ilikuwa ni kutuma kwa njia ya posta. Nakumbuka nikiwa mdogo nilikwenda kwa mama yangu, Mpanda, Rukwa, sasa hivi ni Katavi.

Bahati mbaya mtu aliyetumwa kukata tiketi ya kurejea Dar es Salaam, alipoteza pesa. Mama hakuwa tena na pesa nyingine, wala uwezo wa kuipata.

Kilichofanyika, ni kwamba mimi nikiwa na miaka saba hivi miaka ya katikati ya 1980, ilinibidi niandike barua ili kumfahamisha baba kuwa pesa ya nauli imepotea na anapaswa atutumie nyingine ili kukata tiketi nyingine ya treni kurejea Dar. Hadi zoezi hilo linakamilika, na kuituma, ifike, aipate, atafute tena pesa na kuituma hadi kufika tena, tulitumia mwezi mmoja kukaa tena huko.

Kwa sasa nikikumbuka inabaki ni kumbukumbu isiyofutika kwenye ubongo wangu, hasa nikiona teknolojia ilivyoleta mabadiliko.

Najiambia mwenyewe kama ingekuwa leo, ilikuwa ni kiasi cha kumpigia baba simu na kumwambia kilichotokea na kama angekuwa na pesa, basi angetuma kwenye simu hiyo hiyo, keshokutwa tu tiketi ingepatikana.

Kama angekuwa hana hadi atafute, nadhani muda mrefu sana ingekuwa siku tatu au nne tu.

Haya ndiyo maisha ya wakati huo, bila simu wala teknolojia ya sasa.

Basi ilikuwa ni hivyo hivyo hata kwenye mawasiliano kwenye soka. Watu wengi miaka hiyo kabla ya 1995 , matokeo ya mechi za Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara (sasa Ligi Kuu), Ligi ya Muungano, wengi waliyasikiliza kwenye redio.

Wakati huo redio ilikuwa ni moja tu Redio Tanzania Dar es Salaam, maarufu kama RTD. Kama mpira ukitangazwa Dar, basi viwanja vingine vya mikoani hakuna yoyote anayejua matokeo ya mechi. Kila mmoja atajua ya Dar tu kwa sababu mpira ulikuwa unatangazwa. Basi mechi zingine kujua ni mpaka saa mbili kasorobo wakati wa

**"Kwa sasa nikikumbuka inabaki ni kumbukumbu isiyofutika kwenye ubongo wangu, hasa nikiona teknolojia ilivyoleta mabadiliko."**

kipindi cha michezo.

Mashabiki ukifika muda huo watakusanyana kwenye redio, tena wakati huo wala hazikuwa nyingi, kwa nia tu ya kusikiliza matokeo ya mechi za mikoani. Inawezekana kabisa Yanga au Simba moja wapo itakuwa imecheza mikoani. Mashabiki watataka kusikiliza matokeo.

Watangazaji wa wakati huo walikuwa na mbwembwe sana, vichwa vya habari wataweka mafumbo ambayo kama siyo mwerevu huwezi kung'amua.

"Huko Tanga, usimlaumu dobi, kaniki ndiyo rangi yake, Dodoma mgagaa na upwa hali wali mkavu, Arusha, mgeni njoo mwenyeji apone, Mwanza wapiganapo mafahari wawili ziumiazo ni nyasi," na misemo mingi inayofikirisha, kabla ya kukupa matokeo kamili ya mechi baadaye.

Wakati huo kulikuwa na timu kama Pamba ya Mwanza, CDA ya Dodoma, Mecco ya Mbeya, Tukuyu Stars, RTC Kagera, RTC Kigoma, Biashara ya Mwanza, Nyota Nyekundu, Waziri Mkuu, Kurugenzi Dodoma, Sigara, Milambo ya Tabora, Reli ya Morogoro na nyingine nyingi zilizokuwa zikipanda na kushuka.

Haikuwezekana hata mtu wa Dar es Salaam kujua matokeo hata ya Simba na Reli ikicheza kwenye Uwanja wa Jamhuri Morogoro mpaka saa mbili kasorobo.

Mara chache sana na watu wachache sana ndiyo waliokuwa na uwezo wa kujua, hasa wale wa maofisini, wakiwasiliana na wenzao wa maofisi mengine ya mkoa husika kwa kutumia simu ya mezani, ambapo ilikuwa nadra kwa mashabiki wa kawaida mara zote kupata taarifa hizo. Na hata zikivuja inakuwa kama haziaminiki, hadi kwenye michezo saa mbili kasorobo. Na tetesi hizo huwezi kuzipata kila mechi.

Hebu fikiria kwa sasa kila kitu kiko laivu, mashabiki wanaangalia mechi kwenye televisheni Dar es Salaam, majiji mengine na mikoani akijua kila kitu kinachoendelea. Hata kama kuna shabiki aliingia uwanjani unamuona moja kwa moja. Wakati huo hata kujua matokeo tu ni tabu.

Wakati mwingine hata bingwa wa nchi anakuja kujulikana na kutangazwa kwenye kipindi cha michezo, kama hadi mechi za mwisho timu mbili mpaka tatu zinakuwa na mategemeo ya kutwaa ubingwa.

Siku hizi, hata ukiwa na simu yako ya mkononi ukitaka unaweza kupenyezewa matokeo hata kwa meseji, kama hutaki kusikiliza na kutazama kwenye simu hiyo hiyo.

Wakati kwa sasa watu wakiangalia Ligi mbalimbali za Ulaya, UEFA, EURO, AFCON au Kombe la Dunia laivu, haikuwezekana kabisa wakati huo. Kama matokeo ya mechi za Ligi Kuu mikoani kama mpira hautangazwi huwezi kupata, iweje michuano hiyo?

Bingwa wa AFCON au Ligi ya Mabingwa, hutangazwa kwenye taarifa ya habari, utasikia mtangazaji akisema, "mpira, timu ya Asante Kotoko ya Ghana imetwaa Kombe la Afrika kwa kuifunga Al Ahly ya Misri, bao 1-0 lililofungwa na Opuku Nti." Na hiyo ilikuwa ni siku ya pili au tatu baada ya mechi hiyo kuchezwa. Hiyo ilikuwa mwaka 1983, Waghana hao walipotwaa Ligi ya Mabingwa Afrika. na hali ndivyo ilivyokuwa hivyo miaka yote.

Majuzi tu, tulikuwa tunaangalia AFCON laivu kutoka nchini Cameroon hadi fainali Ivory Coast ikitwaa. Miaka ya nyuma tungesikiliza kwenye taarifa ya habari baada ya siku moja, mbili au tatu.

Wachezaji wa zamani wa Simba kutoka kushoto ni, Jamhuri Kihwelo 'Julio', Idd Pazi na Zamoyoni Mogella, wakiwa kwenye maandalizi ya moja ya mechi zao mwanzoni mwa miaka ya 1990.

**Tuma meseji 0716 350534**

HABARI KIMATAIFA

## Malawi yatangaza ugonjwa wa polio

**LILONGWE,** MALAWI

MALAWI imetangaza kuibuka kwa ugonjwa wa polio na kuwa kisa cha kwanza barani Afrika baada ya miaka mitano, Shirika la Afya Duniani (WHO) limesema.

Mamlaka ya Afya ya Malawi, ilitangaza kuzuka kwa virusi vya polio aina ya type 1 baada ya kisa kimoja kugunduliwa katika mji mkuu Lilongwe.

Virusi vya polio vilimuathiri msichana wa miaka mitatu na kumsababishia kupooza.

Uchunguzi wa kimaabara uligundua kuwa aina hiyo ya virusi ni sawa na ile inayosambaa Pakistan, mamlaka ya afya ilisema.

Afghanistan na Pakistan ndio nchi mbili pekee ambapo polio ya aina hiyo imeenea.

Kisa cha mwisho kinachojulikana cha polio hiyo barani Afrika kilitokea mnamo mwaka 2016 katika jimbo la Borno, Nigeria.

Bara hilo lilitangazwa kuwa halina tena polio ya aina hiyo mwaka 2020.

Virusi hivyo huvamia mfumo wa neva na inaweza kusababisha kupooza kabisa ndani ya masaa machache. **DW**

## Niger yakubali kupokea wanajeshi wa Ufaransa

**NIAMEY,** NIGER

Niger imekubali kuruhusu wanajeshi wa vikosi maalumu kutoka Ufaransa na nchi za Ulaya kupelekwa nchini humo wakitokea nchi jirani ya Mali, ili kulinda eneo la mpaka la nchi hiyo.

Hayo yalielezwa na Rais wa Niger Mohamed Bazoum, kupitia ujumbe wake wa Twitter uliochapishwa jana.

Ujumbe huo ulifafanua kwamba Rais Bazoum, atakuwa tayari kukikabili kitisho cha wanamgambo wa makundi ya itikadi kali katika eneo hilo.

Tamko hilo la kiongozi huyo ni la kwanza tangu Ufaransa ilipotangaza inaondoa majeshi yake nchini Mali pamoja na wanajeshi wa nchi washirika wake.

Kiasi cha wanajeshi 2,400 wa Ufaransa waliokuwa sehemu ya kikosi kilichopelekwa Mali kupambana na makundi yanayofungamana na mtandao wa kigaidi wa Al Qaeda na Dola la Kiislamu, na wengine kiasi 900 wa kikosi maalumu kinachoitwa Takuba.

Wanajeshi hao wanatarajiwa kuondoka Mali katika kipindi cha miezi kadhaa ijayo.

Rais wa Niger, alisema lengo lake ni kuulinda mpaka wake na Mali kwa sababu anaamini makundi ya kigaidi yataimarika na eneo hilo litazidi kuathirika **DW**

# Kijiji chapiga marufuku watu kuzaa

**ACCRA,** GHANA

**Wanawake wajawazito hupelekwa katika vijiji vya jirani wanapotaka kujifungua, hulazimishwa kukaa huko hadi watakapojifungua na watoto wao kukua.**

MAAJABU haya ya dunia! Kwani nchini Ghana kuna kijiji kimoja kinachoitwa Mafi Dove, wakazi wake wote hawajazaliwa eneo hilo baada ya kuwepo kwa sheria ya kupiga marufuku watu kuzaa.

Kijiji hicho ambacho kipo kusini mwa Ghana, kinachukuliwa kuwa eneo takatifu na kuzaa ni moja ya kuchafua.

Kijiji hicho kina watu 5,000, lakini wote hawakuzaliwa huko, kwani moja ya sheria katika eneo hilo inakataza kuzaa, ambako kunachukuliwa kuwa uhalifu dhidi ya miungu.

Wanawake wajawazito hupelekwa katika vijiji vya jirani wanapotaka kujifungua, hulazimishwa kukaa huko hadi watakapojifungua na watoto wao kukua.

Mbali na marufuku ya kuzaa watoto hapo, bado kijiji hicho kina mila mbili zinazofuatwa sana na wakazi hao.

Kwanza ni marufuku kijijini humo kufuga mifugo ambayo bado inaheshimika na wenyeji.

Kwa vyovyote vile, wanyama hao wangeweza kuletwa kijijini na kuchinjwa.

Tamaduni nyingine, ambayo inaonekana kuwa ya kushangaza ni kwamba kijiji hicho hakina makaburi ambapo watu huzikwa.

Wafu katika kijiji hicho wanazikwa kwenye makaburi ya jamii ya vijiji vingine.

**DW**



Kifaru cha kisasa cha Urusi chenye uwezo wa kurusha makombora ya masafa marefu ni miongoni mwa vifaa vilivyokuwa mpakani mwa Ukraine vinavyodaiwa kuondolewa. **PICHA: DW**

# Urusi yaanza kuondoa majeshi yake mpakani

**MOSCOW,** URUSI

Urusi imesema inaendelea kuviondoa vifaru na magari mengine ya kivita kutoka kwenye maeneo ya karibu na mipaka ya Ukraine, baada ya kumaliza mazoezi ya kijeshi.

Taarifa ya wizara ya ulinzi ya Urusi, ilisema mapema jana kwamba treni nyingine iliyobeba wanajeshi, vifaru na vifaa vya kijeshi ambavyo vimepiga kambi eneo la magharibi, imerejea kwenye kambi za kudumu zilizopo mkoa wa Nizhny Novgorod baada ya kukamilika kwa luteka hizo.

Hata hivyo, ilisema kwenye taarifa nyingine kwamba ndege za kivita zilikuwa zikiondolewa kutoka katika rasi iliyonyakuliwa ya Crimea na kupelekwa kwenye viwanja vya ndege katika maeneo mengine, ikiwa ni sehemu ya luteka hizo za kijeshi.

Hatua ya kuendelea kuwapunguza wanajeshi iliyotangazwa jana ni ya karibuni zaidi katika matangazo kadhaa kama hayo yaliyotolewa wiki hii.

Awali nchi hiyo iliibua matumaini ya kupunguza wasiwasi kati ya Urusi na Magharibi katika mgogoro wake na Ukraine, ingawa Marekani ilisema Urusi haijafanya chochote kikubwa na badala yake inazidi kuongeza wanajeshi kwenye mipaka ya Ukraine.

Rais Vladimir Putin, alitarajiwa kusimamia mazoezi hayo hii leo, ambapo atashuhudia mazoezi ya urushwaji wa makombora yatakayofanywa na kikosi maalumu cha nyuklia.

Huku haya yakiarifiwa, Rais wa Belarus Alexander Lukanshenko, tayari aliwasili mjini Moscow kwa ajili ya mazungumzo na mwenyeji wake Rais Putin kuhusiana na hatma ya wanajeshi wa Urusi walioko nchini humo, waliokuwa wakishiriki luteka hizo za kijeshi zilizopangwa kumalizika Jumapili.

Lukashenko alishawahi kusema wazi kuhusu uwezekano wa wanajeshi hao ambao ni sehemu ya wanajeshi wa Urusi waliopiga kambi kaskazini, kusini na mashariki mwa Ukraine kwamba wanaweza kubaki hapo kwa muda mrefu zaidi.

Alisema wamekubaliana kuziacha silaha nchini Belarus na kwamba nchi yake inaweza kuzinunua kutoka Urusi au kuzichukua kama zawadi.

Katika hatua nyingine, mawaziri wa ulinzi wa Urusi Sergei Shoigu na Marekani Lloyd Austin, walitarajia kuzungumza kwa njia ya simu, kuhusu mgogoro huo.

Lakini pamoja na wasiwasi ulioko, nchini Ukraine waziri wa ulinzi wa nchi hiyo Oleksii Reznikov, aliliambia bunge la nchi hiyo kuwa taarifa za kiintelijensia za ndani zinaashiria kwamba kuna uwezekano mdogo wa kusambaa kwa mzozo kati yake na Urusi.

**DW**

# HADITHI

## Operesheni namba moja-14

Mtunzi anapatikana (0716 350534)

**Na Adam Fungamwango**

DIANA ni msichana mrembo kwa maana halisi ya urembo. Na mwenyewe alijijua kuwa ni mzuri wa shani.

Aliwababaisha, kuwaliza, na kuwatia wazimu wanaume wengi ambao alikutana nao, au hata kupishana tu. Wengi walimkimbilia. Wakamtongoza, kumtaka kimapenzi. Wapo waliotaka kumuoa kabisa. Hata hivyo yeye mwenyewe hakujua ni mwanaume gani anayempenda kwa dhati. Alichojua wengi wanamfuata kama nyuki wafuatavyo ua zuri la waridi. Aliacha muda uongee. Alijua mwisho wa siku atajulikana ni nani anayependa uzuri na urembo wake na nani anampenda kwa dhati. Aliyempenda yeye kama yeye na si urembo wake.

Fuatilia mtiririko huu wa riwaya hii kabambe, yenye kusisimua na mafunzo kwa jamii.

********************************

Lengo lilikuwa ni moja. Kufa au kupona. Kuua au kuuawa. Alishajitolea kufa kwa ajili ya Diana. Alimpenda sana Diana. Ni wiki ya pili na siku kadhaa yumo mikononi mwa majahili. Walimteka, wakihitaji pesa kiasi cha shilingi milioni hamsini ili wamuachie. Kwanza ilishindikana pesa zilipowekwa chini ya daraja la Mfugale Tazara, sasa wametaka ziwekwe chini ya daraja la Kajima, lile la kwanza kubwa ukitokea Magomeni kwenda Faya.

Ingawa hakumwambia mjomba wake, lakini safari hii alimwambia rasmi Afande Marco kuhusu jambo hilo ili polisi waende aneo la tukio.

Mara ya kwanza alimwambia, lakini kilichotokea ni kwamba watekaji walijua kilichoendelea na hawakwenda kuchukua mzigo walioahidiwa, lakini safari hii alichobadilisha ni muda.

Kwanza alichoshangaa ni kwa nini watekaji walijua kuwa polisi wamepata taarifa na kushindwa kwenda eneo la tukio.

Ndiyo maana safari hii alimwambia Afande Marco kuwa watekaji wameahidi kufika saa tisa usiku kuchukua mzigo huo. Ni saa moja zaidi kama zilizowekwa na watekaji hao daraja la Mfugale.

Aliwadanganya. Wao huku wakisema ni saa sita. Wala hakuwadanganya polisi kwa bahati mbaya.




Alijua huenda polisi na watekaji wote kabla ya kuja pale huwa wanatanguliza wapelelezi wao. Na huenda ndivyo ilivyotokea mwanzo na watekaji walijua kuwa kuna polisi. Ndiyo maana akaweka masaa matatu mbele. Alijua hata kama polisi kupeleleza watakuja, lakini wanaweza kuanza saa saba. Muda ambao watakuwa wamekuja kufuata mzigo wao. Hapo alichohitaji ni msaada wa polisi.

Tayari ilitimu saa sita na dakika kumi. Alisikia kama kuna watu wanapita kwenye majani katikati ya maji.

Ndiyo. Alimshuhudia mtu mmoja akipita katikati ya maji. Mmoja alipita karibu kabisa na yeye.

Alichokuwa na uhakika nacho ni kwamba watu wale wanaufuata mkoba wa pesa aliouweka sehemu waliyohitaji.

Mmoja alimuona alikuwa anapita karibu yake kabisa. Alijikunja ili asije kuonekana au kukanyagwa na mtu huyo na siri ikajulikana na ikawa hatari kwake, kwani ni dhahiri hawakuwa watu wa mchezo.

Sasa alionekana kufika karibu yake kabisa. Moyo ukaongezeka mapigo. Hakuwa na uhakika kama atabaki hai, pindi mtu yule atakapogundua kuwa kuna mtu mwingine asiyehusika, anashuhudia tukio hilo la wao kuchukua pesa zile.

Ilikuwa ni kama anataka kumkanyaga mguu. Kwa namna ambayo hata mwenyewe hakufikiria, akautoa mguu wake taratibu, bila kuruhusu mtikisiko wowote ambao ungeweza kumshtua. Jamaa alikanyaga pale pale ambapo palipaswa kuwa na mguu wa Jan baada ya kuutoa. Hata hivyo kutokana na giza, wingi wa majani yaliyotengeneza kichaka kinene, hakuonwa.

Fikra ikamjia hapo hapo, akafanye moja kati ya mambo mawili. Baada ya ubongo wake kutafakari kiasi cha robo dakika, akapata maamuzi. Mtu yule alikuwa amefika hatua tatu kutoka alipo. Alichofanya ni kutambaa kwenye tope na majani yake, huku jamaa akiwa anatembea taratibu kwa kunyata na kwa hadhari kubwa.

Kiasi cha hatua moja kabla ya kumfikia, alinyanyuka taratibu na kwa uangalifu mkubwa, kwani alijua chochote kile kitakachomfanya akosee, ataenda kuzimu.

Kwa ustadi wa hali ya juu, akichanganya na mafunzo ya judo, karate na kungfu aliyoyapata, alimrukia shingoni na kumkaba kabali.

Pamoja na kufanya vile, hakutaka mwenzake ashtuke, au kujua kitu chochote kilichompata mwenzake, kwani hiyo ingeweza kumrahishia kazi.

Alinyanyua mguu juu kidogo na

**Kiasi cha hatua moja kabla ya kumfikia, alinyanyuka taratibu na kwa uangalifu mkubwa, kwani alijua chochote kile kitakachomfanya akosee, ataenda kuzimu.**

kuupeleka kwenye mgongo wa mtu yule, huku mikono yake ikijaribu kuirudisha kabali hiyo kwa nyuma.

Alichotaka ni kumpinda mgongo na kumvunja. Jamaa alikuwa mjanja, akakaza. Jan alipoona hivyo akahisi hatari kubwa juu yake kama atapiga kelele kumwita mwenzake. Akaimarisha mkono wake wa kushoto kwenye kabali ile, akiongeza nguvu. Taratibu akaachia mkono wa kulia. Jamaa aliona kama vile Jan anaelekea kushindwa. Hakujua lengo lake. Wakati akitaka kutumia nguvu kuutoa mkono mmoja wa kushoto uliobaki shongoni mwake, alihisi kitu baridi kikipenya chini ya mbavu zake.

Ilikuwa ni kitendo bila kuchelewa, mkono wa kulia wa Jan ulikwenda moja kwa moja kibindoni na kutoa kisu chake. Ni moja kati ya silaha mbili alizokuwa nazo na kuzitegemea kwenye mapambano hayo. Kilichobakia mfukoni ni bastola. Ile aliyoiazima kutoka kwa mjomba Ken.

Sekunde chache baadaye makali ya kisu yalipenya kwenye mwili wa jamaa. Aliguna, lakini si kwa sauti.

Jan alichomoa na kukita tena ndani ya mwili. Safari hii nguvu zilimwishia mtu yule. Akatii kila alichofanya Jan. Alimlaza chini taratibu na kummalizia kwa pigo la tatu.

Ingawa hakutaka mwezake asikie, lakini kishindo kidogo kilisikika, ambacho kilimfanya mtu wa pili kugeuka nyuma. Hakuona kitu.

Tayari mwili wa mwenzake ulikuwa umelala chini kwenye majani, huku Jan pia akilala kifudifudi.

“Nilikwambia Sele, usipite huko, angalia unavyojikwaakwaa, utanikuta mbele.” Sauti ya mwenzake ilisikika.

Jan alitulia tuli. Alijua kuwa sasa amebaki mmoja. Hata hivyo hakujidanganya kama ni kweli amebaki yeye tu. Alichodhani ni kwamba ni lazima kutakuwa na watu wengine. Ama wanafuatilia mwenendo wote, au wanasubiri mzigo na hasa juu ya daraja.

Hata hivyo alijipongeza kwa wazo lake hilo, kwani wazo la pili ilikuwa ni kumuacha kupambana nao, baada ya kuchukua mkoba wa pesa. Aliliona halina maana, ndiyo maana akaamua kummaliza.

Akili yake ilianza kufanya kazi haraka sana kwani tayari kama ni kazi, alikuwa ameshaingia kazini.

Kummaliza wa pili ilikuwa nia yake. “Kama atachukua mkoba na kurudia huku itakuwa ni kazi rahisi sana. Lakini akitokea upande wa pili utakuwa ni mtihani.” Alijiambia huku akimshuhudia mtu aliyebaki akiwa amefika kwenye mkoba, ambao uliwekwa chini ya nguzo ya katikati ya daraja hilo la Kajima.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# TEMBO WARRIORS YAANZA HESABU KOMBE LA DUNIA

Na Saada Akida

TIMU ya Soka ya Taifa ya watu wenye ulemavu (Tembo Warriors), inatarajia kuingia kambini leo jijini Dar es Salaam ili kujiandaa na fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika baadaye mwaka huu.

Tembo Warriors wanatarajia kukaa kambi ya muda wa miezi mitatu.

Baada ya kumalizika kambi hiyo ya miezi mitatu hapa jijini, kikosi hicho kitahamia katika mikoa ya baridi kwa ajili ya kuzoea hali ya hewa ya Uturuki ambapo fainali hizo zitafanyika kuanzia Oktoba 1 hadi 9, mwaka huu katika jiji la Istanbul.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Katibu wa Shirikisho la Soka la Watu wenye ulemavu Tanzania (TAFF), Mosses Mabula, alisema timu hiyo itakuwa na kambi za awamu tatu kabla ya kuanza safari ya kuelekea Uturuki.

**Mabula alisema kambi ya kwanza ilikuwa ya siku mbili ambayo ilianza juzi na jana ambapo wachezaji walikuwa wanafanya mazoezi wakitokea nyumbani na leo kikosi hicho ndio kitaingia rasmi kambi ya kulala pamoja.**

"Hiyo kambi itakuwa ya miezi mitatu na baada ya hapo tutaenda mikoa ya baridi, tunategemea kwenda kati ya Arusha au Karatu na kukaa huko hadi Septemba mwishoni ambapo tutaanza safari kwenda Uturuki na tayari kwa ajili ya michuano hiyo," alisema Mabula.

Aliongeza kuhusu suala la kuboresha benchi la ufundi mchakato bado unaendelea na kwa sasa wamefanikiwa kumwongeza, Ivo Mapunda kwa ajili ya kusaidia kuwanoa makipa wa timu hiyo.

"Kocha Mkuu tayari kila kitu kimeenda vizuri, tumemalizana na kocha, Evren (anamjua kwa jina moja), ambaye alikuwa kocha wa klabu ya Azmir BBK ya Uturuki lakini pia amewahi kuwa kocha msaidizi wa Timu ya Taifa ya Morocco (Amputee)," alisema Mabula.

Kiongozi huyo alisema TAFF kwa kushirikiana na serikali kupitia wizara husika ya michezo wako katika hatua za mwisho kuhakikisha kocha huyo anatua nchini kusaini mkataba na kuanza ajira yake mpya ya kuinoa Tembo Warriors.

Timu hiyo ilipata tiketi ya kushiriki fainali hizo za dunia baada ya kumaliza katika nafasi ya nne kwenye mashindano ya Afrika ambayo yalifanyika hapa nchini mwaka jana.

Rais, Samia Suluhu Hassan, aliahidi kuisaidia timu hiyo katika maandalizi yake ili iweze kwenda kushindana vyema kwenye fainali hizo na kuitaka iingie kambini mapema.



Mshambuliaji wa Azam FC, Prince Dube (kushoto), akijaribu kumtoka mchezaji wa Pamba inayoshiriki Ligi ya Championship katika mechi ya kirafiki iliyofanyika kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza juzi. Azam ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# *Simba SC yaipa jeuri Dar City*

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Dar City inayoshiriki Ligi ya Championship imesema licha ya kubugizwa mabao 6-0 na Simba katika mechi ya michuano ya Kombe la FA hivi karibuni, mchezo huo uliwasaidia vitu mbalimbali ambavyo sasa vinaibeba timu yao.

Uongozi wa Dar City umesema sasa hivi timu yao inajulikana kila wanapopita, jina la klabu yao limekuwa lakini uliwajenga wachezaji wao ambapo bado wanashika nafasi ya pili kwenye kundi lao.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Dar City, Manyolii Manyolii, alisema baada ya kucheza na Simba, wamekuwa maarufu sana kila wanapopita na imefika wakati wanapewa kipaumbele kwa basi lao kuachiwa njia kwa kutokaa foleni.

"Pamoja na kufungwa, lakini ile mechi imetubeba sana, sasa hivi tunaposafiri au kwenda kucheza mechi, hatukai foleni, wakiona tu chata ya Dar City, madareva na hata watu wengine wanaosimamia, wanatupisha na kututania, nyinyi wazee wa sita piteni," alisema Manyolii.

Aliongeza faida nyingine waliyoipata ni kuonekana timu yao ni kubwa kiasi hata wachezaji mitaani au sehemu nyingine wakijitambulisha kama wanachezea Dar City, wanaheshimika.

"Pamoja na kwamba kwa sasa tunakuwa na mechi ngumu, kwani timu zote zikicheza na Dar City zinakamia, lakini imetusaidia sana kujiamini kwa wachezaji wetu kiasi kwamba tumeshinda mechi zote nyingi na sasa tunashika nafasi ya pili nyuma ya Lipuli na tuna uhakika wa kupanda kucheza Championship msimu ujao," aliongeza msemaji huyo.

## KMKM yatamba ikiwakabili Sailor

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

LICHA ya ushindani na ugumu kuongezeka katika Ligi Kuu Zanzibar, vinara wa ligi hiyo, KMKM wamesema bado haijavuruga mipango yao ya kutetea ubingwa wa msimu huu wa mwaka 2021/2022.

KMKM inatarajia kukutana na Black Sailor katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa leo kuanzia saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Amaan.

Kocha Mkuu wa KMKM, Ame Msimu, alisema mechi zote za mzunguko wa 19 ni ngumu kwa sababu kila timu inayoshiriki ligi hiyo imejipanga kupata matokeo chanya na ili kufikia malengo yake.

"Kila timu inayoshuka dimbani imejipanga kuondoka na alama tatu, timu zote hazitaki kuharibu mipango yake ikiwamo ya kutwaa ubingwa na zile zenye lengo la kubaki ligi kuu," alisema kocha huyo. Alisema anautazama mchezo wake huo kuwa ni mchezo mgumu kwakuwa wapinzani wao nao wanahitaji alama tatu ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kubaki ligi kuu ya Zanzibar.

"Tunapambana ili tunyakuwe ubingwa, tunajua safari bado ndefu, tunahitaji kushinda mechi zetu zote za mzunguko huu wa lala salama lakini pia waliopo chini yetu pia wanahitaji kushinda, hivyo mpambano bado ni mkali, matumaini yetu ni kutimiza malengo," alisema Msimu.

Aliongeza mbali na kutwaa ubingwa, zawadi mbalimbali zinazotarajiwa kutolewa na wadhamini wa ligi hiyo, benki ya PBZ, pia zimechochea kila timu kujipanga kuziwania, tofauti na ilivyokuwa msimu ya nyuma.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa leo zitakuwa ni kati ya Machomane dhidi ya Kisiwani ambayo itachezwa kwenye Uwanja wa Gombani, Pemba wakati saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Amaan Maafande wa Polisi watawakaribisha Yosso Boys.

KMKM inaongoza Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na pointi 39 na inafuatiwa na Mafunzo yenye pointi 36 wakati JKU yenye pointi 36 pia inashika nafasi.

## ZISIKUPITE

### MBAPPE KUTUA LIVERPOOL

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 23, inaaminika kubadili upepo kuelekea Liverpool baada ya kutohamasika na kiwango kilichoonyeshwa na Real Madrid katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Paris St-Germain. (***Sport, via Star***)

### MBAPPE KUIKAMUA PSG

KLABU ya PSG ipo tayari kumfanya, Kylian Mbappe (23), kuwa mchezaji anayelipwa fedha nyingi zaidi duniani kwa kumpa mshahara unaokaribia pauni milioni moja kwa wa wiki ili kumzuia asiondoke. (***Independent***)

### RONALDO KUMFUATA MESSI

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37 anaweza kujikuta akicheza pamoja na mpinzani wake, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 34, msimu ujao pale Paris St-Germain. (***Mirror***)

### KIERAN ATAKIWA MADRID

REAL Madrid inajipanga kumsajili mlinzi wa kushoto wa Arsenal raia wa Scotland, Kieran katika dirisha la usajili ya majira ya joto. (***Calciomercato, via Sun)***

### SAVIO KUTUA CITY

KLABU ya Manchester City inakaribia kumsajili winga wa kibrazil, Savio kutoka Atletico Mineiro, tayari siku ya kufanyiwa vipimo vya afya kwa kinda huyo mwenye umri wa miaka 17 imepangwa. (***Fabrizio Romano***)

### RICE MAMBO MAGUMU

MATUMAINI ya kiungo wa West Ham na England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 23 ya kujiunga Chelsea yamefifishwa baada ya kocha, Thomas Tuchel kuamua kumtumia kiungo, Conor Gallagher (22), kwenye kikosi cha kwanza cha 'Blues' msimu ujao. (***Standard***)

### CARLOS ANUKIA EPL

KLABU ya Newcastle ipo tayari kupeleka ofa mpya kwa ajili ya mlinzi wa Sevilla, Mbrazili Diego Carlos ambaye ana umri wa miaka 28. (***Marca, via Sun***)

### ARSENAL, CITY VITANI

ARSENAL na Manchester City zinafikiria kumsajili mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez mwenye umri wa miaka 24 katika dirisha lijalo la usajili. (***Sun***)

### MARSCH KUMRITHI BIESLA

BOSI wa zamani wa Red Bull Salzburg na RB Leipzig, Jesse Marsch ni chaguo la kwanza la Leeds United kuchukua nafasi ya kocha, Marcelo Bielsa mwenye umri wa miaka 66, kama klabu hiyo itaamua kuachana na kocha huyo raia wa Argentina mwishoni mwa msimu. (***Telegraph)***

### DOKU ANUKIA NEWCASTLE

NEWCASTLE United inamfuatilia kwa karibu kinda wakimataifa wa Ubelgiji, Jeremy Doku mwenye umri wa miaka 19 ambae anachezea Rennes akitajwa kuwa na thamani ya pauni milioni 22. (***Chronicle***)

### BOTMAN SOKONI EPL

BAADA ya majaribio kadhaa ya kumsajili mlinzi, Sven Botman mwenye umri wa miaka 22 kutoka Lille katika dirisha la usajili la Januari, Newcastle United imeanza mazungumzo ili kupata huduma yake katika dirisha lijalo la usajili. (***Mirror***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# LIVERPOOL NI KUSUKA AU KUNYOA KWA SALAH

**Wakifanikiwa kumbakisha ataweka rekodi ya kulipwa mshahara mkubwa zaidi...**

**LIVERPOOL,** ENGLAND

LIVERPOOL wanaweza kuwa na chaguo gumu la kufanya msimu huu wa joto kwa mshambuliaji wao, Mohamed Salah.

Nyota huyo wa kimataifa wa Misri, Salah amebakiwa na chini ya miezi 18 katika mkataba wake wa sasa unaomfanya alipwe mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki, huku Juni, mwaka huu atafikisha umri wa miaka 30.

Klabu hiyo hadi sasa haina chaguo, kwani ikahitaji kumwacha aondoke ikiwa wataepuka kupoteza bure mwaka wa 2023.

Salah ni mmoja wa wachezaji bora kwenye Ligi Kuu England na Liverpool hawatataka kumwona akiondoka, lakini wanaweza kulazimika kumfanya kuwa mchezaji wa kwanza kabisa kwenye soka la Uingereza anayelipwa pauni 500,000 kwa wiki.

**Mshahara ambao ungezidi hata ule wa mchezaji wa Manchester United, Cristiano Ronaldo, ambaye anapokea kiasi cha pauni 480,000 kwa wiki.**

Mchezaji huyo alikiri hivi majuzi kwa jarida la GQ: "Nataka kubaki, lakini haiko mikononi mwangu. Iko mikononi mwao. Wanajua ninachotaka. Siombi mambo ya kichaa."

Lakini Liverpool wanaweza kuhitaji kuanza kupanga maisha ya baadaye bila yeye ikiwa hawawezi kukubaliana na masharti mapya.

Usajili wa klabu katika misimu ya hivi majuzi umekuwa wa kustaajabisha, ambapo Januari walimsajili winga, Luis Diaz kwa pauni milioni 37.5.

Pia Harvey Elliott mwenye umri wa miaka 18 alirejea kutokana na majeraha kukiwapa chaguo zaidi.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 940
MECHI KALI
MANCHESTER CITY
VERSUS
TOTTENHAM
1 | 1.34
X | 5.12
2 | 8.59
PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# RAIS LALIGA AMWITA MBAPPE



**MADRID,** Hispania

RAIS wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Javier Tebas, anaamini nyota wa Paris Saint-German, Kylian Mbappe atajiunga na Real Madrid mwishoni mwa msimu huu.

Mbappe, ambaye alifunga bao la dakika za lala salama dhidi ya Madrid katika mechi ya kwanza kwa hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumanne, mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu na amekuwa akihusishwa na kutaka kuhamia Santiago Bernabeu.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia ana mabao 22 na asisti 13 katika michezo 32 katika michuano yote aliyoichezea PSG msimu huu na alisema baada ya ushindi wa 1-0 dhidi ya Madrid bado hajaamua juu ya mustakabali wake, huku klabu hiyo ya Paris ikiripotiwa tayari kupambana kumbakiza.

Lakini akizungumza na waandishi wa habari, Tebas alionyesha imani yake kwamba Mbappe atacheza soka lake kwenye LaLiga kuanzia msimu ujao, ikiwezekana akiwa na mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Haaland, ambaye Los Blancos pia wanahusishwa naye.

"Madrid itawapata Mbappe na Haaland kwani wengine (Barcelona na Juventus) wana matatizo ya kifedha," alisema.



# Xavi amlinganisha Torres na Suarez

**BARCELONA,** Hispania

XAVI ana uhakika Ferran Torres atakuwa na wakati mzuri zaidi Barcelona licha ya kuanza maisha kwa shida hapo Camp Nou.

Torres, aliyesajiliwa Desemba mwaka jana akitokea Manchester City, aliokoa sare ya bao 1-1 kwa Barca nyumbani dhidi ya Napoli kwenye Ligi ya Europa, akifunga kwa mkwaju wa penalti.

Hata hivyo, hilo lilikuwa jaribio la pekee kati ya majaribio tisa ya fowadi huyo kulenga shabaha siku ya Alhamisi alipopata mfululizo wa fursa nyingi za kufunga, akionekana kukaribia kutokwa na machozi muda wote baada ya kukosa nafasi ya wazi dakika ya mwisho.

Katika mechi sita za mashinda[...] yote alizoichezea Blaugrana h[...] hadi sasa, Torres amefunga ma[...] mbili.

Lakini mabao hayo yametoka[...] na mashuti yake mawili pekee ya[...] yolenga lango, huku majaribio me[...]gine 15 yakishindwa kuwasumb[...] makipa wa timu pinzani.

Hata hivyo, kocha Xavi anaam[...] kuwa haya yote ni sehemu ya m[...]sha ya Barcelona, akilinganis[...] mazingira ya Torres na ya Luis S[...]arez baada ya uhamisho wake w[...] mwaka 2014 kutoka Liverpool.

Suarez, alitoka katika msimu w[...] mabao 31 kule Anfield, alifun[...] mara moja tu katika mechi za[...] nane za kwanza kwa klabu ya[...] mpya.

## HABARI MICHEZO

,850,660

JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/02/22 | 18:00 | Zaragoza vs Las Palmas UD | 2.80 | 3.19 | 2.44 |
| 02. 19/02/22 | 18:00 | Luton Town vs West Bromwich | 2.74 | 3.03 | 2.59 |
| 03. 19/02/22 | 19:00 | Lens vs Lyon | 2.75 | 3.40 | 2.46 |
| 04. 19/02/22 | 20:30 | Oostende vs Standard Liege | 2.55 | 3.34 | 2.60 |
| 05. 19/02/22 | 20:30 | Cadiz CF vs Getafe | 3.05 | 2.95 | 2.55 |
| 06. 19/02/22 | 21:00 | Niort vs AJ Auxerre | 2.70 | 2.95 | 2.70 |
| 07. 20/02/22 | 13:30 | Gaziantep BB vs Adana Demirspor | 2.58 | 3.27 | 2.63 |
| 08. 20/02/22 | 14:15 | PEC Zwolle vs Groningen | 2.38 | 3.24 | 2.85 |
| 09. 20/02/22 | 14:30 | Fiorentina vs Atalanta | 2.85 | 3.45 | 2.38 |
| 10. 20/02/22 | 16:00 | Fatih Karagumruk vs Sivasspor | 2.60 | 3.19 | 2.65 |
| 11. 20/02/22 | 17:00 | Venezia vs Genoa | 2.55 | 3.21 | 2.80 |
| 12. 20/02/22 | 18:30 | Maritimo vs Famalicao | 2.39 | 3.26 | 2.86 |
| 13. 20/02/22 | 19:30 | Wolverhampton vs Leicester | 2.42 | 3.15 | 3.05 |

MECHI ZA USHINDI
"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 19/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 3110 | Polisi Tanzania vs Kagera Sugar | 2.34 | 2.60 | 3.47 |
| 15:30 | 5651 | West Ham vs Newcastle | 1.68 | 3.95 | 4.71 |
| 16:00 | 5213 | Kayserispor vs Giresunspor | 2.29 | 3.16 | 3.11 |
| 17:00 | 1865 | Liptovsky Mikulas vs Ruzomberok | 3.85 | 3.56 | 1.79 |
| 17:00 | 3213 | MSK Zilina vs Zemplin Michalovce | 1.29 | 5.00 | 8.08 |
| 17:00 | 4893 | FK Pohronie vs Slovan Bratislava | 12.50 | 5.96 | 1.17 |
| 17:00 | 5404 | Spartak Trnava vs AS Trencin | 1.35 | 4.71 | 6.92 |
| 17:30 | 5355 | VfL Wolfsburg vs Hoffenheim | 2.65 | 3.49 | 2.50 |
| 17:30 | 5460 | Augsburg vs SC Freiburg | 2.89 | 3.33 | 2.39 |
| 17:30 | 5523 | Arminia Bielefeld vs Union Berlin | 2.97 | 3.17 | 2.42 |
| 18:00 | 1572 | Crystal Palace vs Chelsea | 5.19 | 3.84 | 1.65 |
| 18:00 | 1581 | Preston vs Reading | 1.66 | 3.68 | 4.90 |
| 18:00 | 1613 | Southampton vs Everton | 2.06 | 3.55 | 3.40 |
| 18:00 | 1642 | Cardiff vs Blackpool | 2.12 | 3.20 | 3.39 |
| 18:00 | 2158 | Hibernian vs Ross County | 1.84 | 3.39 | 4.23 |
| 18:00 | 2334 | St Johnstone vs Hearts | 4.04 | 3.30 | 1.90 |
| 18:00 | 2469 | Brighton vs Burnley | 1.67 | 3.64 | 5.39 |
| 18:00 | 2552 | Liverpool vs Norwich City | 1.11 | 9.00 | 20.99 |
| 18:00 | 3253 | Motherwell vs Aberdeen | 3.06 | 3.01 | 2.41 |
| 18:00 | 3657 | Crusaders Belfast vs Carrick Rangers | 1.22 | 5.59 | 9.63 |
| 18:00 | 3944 | Aston Villa vs Watford | 1.60 | 3.99 | 5.38 |
| 18:00 | 4022 | Arsenal vs Brentford | 1.49 | 4.13 | 6.77 |
| 18:00 | 5787 | Livingston vs St Mirren | 2.23 | 3.10 | 3.29 |
| 18:15 | 2069 | Osasuna vs Atletico Madrid | 3.60 | 3.25 | 2.11 |
| 18:15 | 5089 | Ionikos Nikea FC vs OFI Crete | 2.71 | 2.96 | 2.71 |
| 18:30 | 3481 | Hapoel Beer Sheva vs Ironi Kiryat Shmona | 1.45 | 4.03 | 6.15 |
| 19:00 | 1700 | Hapoel Katamon vs FC Ashdod | 3.05 | 3.10 | 2.23 |
| 19:00 | 2948 | Lens vs Lyon | 2.74 | 3.44 | 2.44 |
| 19:00 | 3749 | Josko Ried vs WSG Wattens | 2.27 | 3.38 | 2.75 |
| 19:00 | 5368 | Austria Vienna vs TSV Hartberg | 1.74 | 3.67 | 3.96 |
| 19:00 | 5533 | Admira Wacker vs LASK Linz | 3.95 | 3.57 | 1.76 |
| 19:00 | 5859 | Besiktas vs Altay | 1.45 | 4.45 | 6.14 |
| 20:00 | 3008 | FC Lugano vs St. Gallen | 2.40 | 3.30 | 2.81 |
| 20:00 | 3421 | FC Wil vs FC Schaffhausen | 2.61 | 3.48 | 2.33 |
| 20:00 | 3928 | Roma vs Verona | 1.88 | 3.74 | 3.84 |
| 20:00 | 4185 | SC Kriens vs FC Aarau | 3.85 | 3.66 | 1.76 |
| 20:30 | 1012 | FC Koln vs Eintracht Frankfurt | 2.26 | 3.62 | 2.88 |
| 20:30 | 2911 | Panetolikos vs Panathinaikos | 4.35 | 3.17 | 1.89 |
| 20:30 | 3093 | Atromitos vs Asteras Tripolis | 3.15 | 3.00 | 2.35 |
| 20:30 | 5017 | Cadiz CF vs Getafe | 3.10 | 2.90 | 2.55 |
| 20:30 | 5240 | Manchester City vs Tottenham | 1.34 | 5.12 | 8.59 |
| 20:45 | 1474 | Willem II Tilburg vs Ajax | 24.53 | 9.61 | 1.07 |
| 20:50 | 4783 | Hapoel Hadera vs Beitar Jerusalem | 2.31 | 3.12 | 2.88 |
| 21:00 | 1690 | Pacos Ferreira vs FC Vizela | 2.35 | 3.16 | 3.01 |
| 22:30 | 5448 | FC Basel vs Lausanne-Sport | 1.48 | 4.55 | 5.54 |
| 22:45 | 2311 | Sligo Rovers vs Bohemians FC | 3.22 | 3.12 | 2.13 |
| 22:45 | 3134 | Salernitana vs AC Milan | 7.57 | 4.98 | 1.38 |
| 23:00 | 1288 | Real Madrid vs Alaves | 1.26 | 5.74 | 10.78 |
| 23:00 | 4338 | Nantes vs Paris St Germain | 5.63 | 4.32 | 1.52 |
| 23:30 | 3782 | Vitoria Guimaraes vs FC Arouca | 1.78 | 3.54 | 4.33 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# AZAM YAITUMIA SALAMU BIASHARA IKITEMA CHECHE

**Shufaa Lyimo na Adam Fungamwango**

WAKATI Azam FC juzi ilipata ushindi wa mabao 2-0 katika mechi ya kirafiki dhidi ya Pamba, uongozi wa Biashara United umesema kikosi chao kimeimarika kwa ajili ya kuwakabili 'Wanalambalamba' katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Jumanne.

**Mabao ya Azam katika mechi hiyo yalifungwa na wachezaji wake wa kigeni, Mzambia Rodgers Kola na Prince Dube kutoka Zimbabwe.**

"Maandalizi yanakwenda vizuri kuelekea kwenye mchezo wetu wa Ligi Kuu dhidi ya Biashara United, kwa sasa tuko Mwanza tumeweka kambi hapa kwa sababu mbalimbali, ikiwamo kuhamasisha mashabiki wetu na tumetembelea tawi la klabu yetu lililopo Igogo sokoni. Lengo ni kuhamasisha na kuwafanya mashabiki kuzidi kuipenda na kuifuatilia Azam FC, " alisema Thabit Zacharia maarufu kama Zaka Zakazi, Ofisa Habari wa klabu hiyo.

Naye Meneja wa Biashara United, Frank Wabare, alisema kikosi chao kinaendelea vizuri kuelekea katika mchezo huo na wamejipanga kuzibakisha pointi tatu nyumbani.


"Wachezaji wanaendelea na mazoezi kwa ajili ya kukutana na Azam, tunajua utakuwa mchezo mgumu na wenye ushindani," alisema Wabare.

Alisema baada ya kutolewa kwenye mashindano ya Kombe la FA na Yanga, sasa hivi nguvu zao wamezielekeza katika mchezo huo na wanaamini hawatarudia makosa ambayo yaliwaondoa kwenye michuano hiyo inayochezwa kwa mfumo wa mtoano.

Meneja huyo amewataka mashabiki wao waendelee kuwaunga mkono ili wafanye vizuri katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara kwa ajili ya kutimiza malengo yao na wanaamini uwezo wa kuyafikia wanao.

Aliongeza wanaupa umuhimu mkubwa mchezo huo kwa sababu wanafahamu msimu huu hakuna timu ya kubeza kutokana na maandalizi yaliyofanywa wakati wa usajili.

Azam yenye pointi 24 iko katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi baada ya kucheza mechi 14 sawa na Biashara United yenye pointi 12 na iko katika nafasi ya 13.




Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tulia Ackson, akifurahia jezi ya Yanga aliyokabidhiwa baada ya kuwa mgeni rasmi kwenye hafla ya uzinduzi wa kadi mpya za uanachama wa klabu hiyo kwa njia ya kielektroniki uliofanyika kwenye bunge hilo jijini Dodoma jana. **PICHA: MTANDAO**

# *Champion wa Kitaa ulingoni*

**Na Saada Akida**

HATUA ya pili ya mashindano ya kusaka Nyota wa Mtaa (Champion wa Kitaa), yamepangwa kufanyika kesho kwenye Ukumbi wa Dar Live ulioko Mbagala jijini Dar es Salaam.

Mratibu wa mashindano hayo kutoka Peaktime Media, Meja Selemani Semunyu alisema malengo ya shindano hilo ni kukuza vipaji vya masumbwi kwa mabondia chipukizi walioko mitaani ambao wamekosa nafasi ya kuonyesha vipaji vyao.

Semunyu alisema mtaani kuna vijana wengi wenye uwezo wa kucheza mchezo wa ngumi lakini hawana sehemu ya kuonyesha vipaji vyao na mashindano hayo yatasaidia kuwatambulisha na kuwaendeleza ambapo baadaye watapeperusha bendera ya nchi kimataifa.

"Tulianza shindano hilo kwa awamu ya kwanza ilikuwa Jumapili iliyopita ambapo yalifanyika Tandika jijini Dar es Salaam, kwa kupata mabondia 10 ambao kesho (leo) watapima uzito kwa ajili ya mchezo wa hatua ya pili ya kutafuta bingwa wa kitaa," alisema Semunyu.

Aliwataja mabondia ambao watacheza hatua ya pili ni Omary Matimbwa dhidi ya Bakari Kitogo, David Edward atachuana na Adam Sega, Saidi Uwezo atapambana na Saidi Mohamed, Enock Enock yeye ataonyeshana nguvu na Said Ndilimo.

Mabondia wengine ni Sebastiani Deo vs Amour Sheikh Hajj, Peter Tosh vs Ramadhan Msham huku Jadi Salehe watarudiana na Hussein Mkalekwa ambao wiki iliyopita walitoka sare.

# Michezo

Jumamosi Februari 19, 2022

Nipashe





Liver kusuka au kunyoa kwa Salah UKURASA 21



Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson (kushoto), akimkabidhi kadi ya uanachama wa Yanga ya kielektroniki Mwenyekiti wa Baraza la Wadhamini wa klabu hiyo, George Mkuchika katika hafla fupi iliyofanyika jijini Dodoma jana. **PICHA: MTANDAO**

## Mtibwa yapanga kuivuruga Yanga

**Na Shufaa Lyimo**

MUDA utazungumza, hii ni baada ya kila upande kati ya wageni Yanga na Mtibwa Sugar kutamba timu yake itaondoka na ushindi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Jumatano kwenye Uwanja wa Manungu, Turiani mkoani Morogoro.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ya Yanga, Thabit Kandoro, aliliambia gazeti hili uongozi wa timu hiyo unashirikiana vyema na wachezaji pamoja na benchi la ufundi ili kuhakikisha wanapata ushindi katika mchezo huo.

"Maandalizi yanaendelea vizuri, hatupoi tupo mbio kwenye harakati za kutwaa Kombe la FA na ubingwa wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara," alisema Kandoro.

Mwenyekiti huyo aliongeza kuwa Yanga ni timu kubwa na yenye wachezaji wenye viwango vizuri, hivyo wanaamini watafanya vyema katika kila mchezo wanaocheza.

Aliongeza ingawa wanafahamu mchezo huo dhidi ya Mtibwa Sugar utakuwa mgumu kutokana na historia ya kila mara wanapokutana, wamejiandaa kukutana na changamoto mbalimbali.

"Tunawaheshimu sana wapinzani wetu japo kuwa hawajafanya vizuri katika michezo iliyopita, wanapokuwa kwao mchezo unakuwa mgumu, hutukamia," Kandoro alisema.

Kiongozi huyo alisema mechi zote msimu huu ni ngumu na kila timu haitaki kupoteza hata mchezo mmoja kwa sababu itawaondoa kwenye mipango ya kufikia malengo.

Naye Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Salum Mayanga, alisema makosa ambayo aliyabaini katika mchezo wa Kombe la FA dhidi ya Coastal Union ameyafanyia kazi na anaamini wataikabili Yanga tofauti.

Mayanga alisema mechi hiyo ni muhimu zaidi kwake kwa sababu anahitaji kujinasua mkiani na aliweka wazi atamkosa beki, Ibrahim Ame, ambaye aliumia goti kwenye mchezo uliopita dhidi ya Coastal Union.

# Simba yazipigia hesabu pointi 6

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

### ●●● Yasema imedhamiria kuendelea kuiwakilisha nchi vizuri ingawa...

KIKOSI cha wachezaji 23 pamoja na benchi la ufundi la Simba kiliondoka nchini jana kuelekea Niger huku kikisema dhamira yao ni kuendelea kupata matokeo mazuri katika mechi mbili zinazofuata za Kundi D kwenye michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

**Simba imesema inakwenda ugenini Niger na Morocco kuchukua pointi sita ili kujiimarisha katika kilele cha kundi lao ambalo sasa linaongozwa na RS Berkane ya Morocco.**

US Gendarmarie inatarajia kuikaribisha Simba kesho katika mechi ya pili itakayochezwa kwenye Uwanja wa Jenerali Senyi Kountch uliopo Niamey kuanzia saa 1:00 usiku kwa saa za Tanzania (sawa na saa 11:00 jioni huko Niger).

Akizungumza na gazeti hili Dar es Salaam kabla ya kupanda ndege jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kikosi cha Wekundu wa Msimbazi hakitakuwepo Tanzania kwa muda wa siku 10 kwa ajili ya majukumu ya kimataifa waliyokuwa nayo.

Ahmed alisema Simba imejiandaa vizuri kuelekea michezo hiyo miwili ya ugenini kwa kutarajia kurejea na pointi sita au nne kama mambo yatakwenda tofauti na mipango yao.

Alisema baada ya kumaliza mechi dhidi ya US Gendarmarie hapo kesho, kikosi hicho kinachofundishwa na Mhispania Pablo Franco kitaifuata mapema RS Berkane kwa ajili ya mchezo wake wa tatu utakaochezwa Februari 27, mwaka huu.

"Tunaamini utakuwa mchezo mgumu, tunahitaji kupata pointi tatu, tunaenda kucheza mchezo huo tukiwa na kumbukumbu nzuri ya ushindi wa mabao 3-1 tuliyopata katika mechi ya kwanza nyumbani dhidi ya Asec Mimosas,"alisema Ahmed.

Aliongeza wanakwenda kupambana kuitetea bendera ya Simba lakini pia wanafahamu katika michuano hiyo kwa sasa wanapeperusha bendera ya Tanzania na Afrika Mashariki.

"Tutakuwa na kambi ya siku nne hapo Niger, halafu Februari 25, mwaka huu tutaendelea na safari kuelekea Morocco kwa ajili ya mchezo wetu wa tatu dhidi ya RS Berkane, kwa maandalizi waliyoyapata wachezaji wetu tunatarajia kurejea na pointi zisizopungua nne katika michezo hiyo," Ahmed alisema.

Aliongeza kocha wao (Franco) amefanya maandalizi ya kuwasoma wapinzani wao na ana imani suala la kiufundi kuhusiana na kuwakabili waarabu hao linaendelea vizuri na matarajio ni kupata matokeo mazuri katika michezo hiyo miwili.

"Tunakwenda na hahadhari, ndiyo maana tumetuma wajumbe watangulie ili kuweka kila kitu sawa huko kuanzia kambi, chakula na viwanja vya mazoezi, USGN imepoteza mechi yake ya kwanza, hivyo tunajua haitokubali kupoteza mechi ya pili kirahisi, lakini pia haitokubali kupoteza mechi ikiwa nyumbani, hayo yote tunayajua," alisema kiongozi huyo.

Alisema pia Simba iko tayari kucheza mechi katika mazingira ya aina yoyote kwa sababu wana uzoefu na michuano hiyo na kuongeza wameshawahi kucheza kwenye mazingira tofauti, hivyo haiwapi shida.

Aliwataja wachezaji waliobaki wote ni majeruhi, ambao ni Chris Mugalu, Kibu Denis na Hasaan Dilunga lakini akisema pia watarejea nyumbani Februari 28 kwa ajili ya kujiandaa kuwavaa Biashara United katika mchezo mwingine wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Machi 3, mwaka huu.

RS Berkane ndio vinara wa Kundi D baada ya kupata ushindi wa mabao 5-3 katika mchezo wake wa kwanza walipowavaa US Gendarmarie inayoburuza mkia kwenye kundi hilo.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED,S L P

9 770856 541002 >